**Sababu** wanaume kuoa wake wengi zawekwa bayana



UKURASA 5

**Watoto** kuzaliwa kabla ya wakati mtihani mgumu



UKURASA 3

**Israel** yakiri haikufanikiwa kupunguza vifo kwa raia Gaza

UKURASA 17


# Nipashe

Jumamosi Novemba 18, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581498

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




**SON AWATOA HOFU MASHABIKI TOTENHAM SPURS**

UKURASA 22

BAA LA KISUKARI

# Kila sekunde 20, mguu unakatwa

• **Wataalamu** Muhimbili, wizara waanika hali ilivyo... *Ukurasa 4*



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa amesimama pamoja na Mgeni wake Rais wa Romania, Klaus Iohannis baada ya kuwasili Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Tanzania, Romania zaweka mkakati sekta za afya, elimu

UKURASA 2

# Hoja sita zilizombeba Sabaya kushinda kesi

• **Majaji** washtuka jambazi kupeleka polisi waathirika wa tukio la uhalifu... *Ukurasa 2*



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, akipongezana na mawakili wake baada ya kushinda rufani ya kesi ya jinai namba 105 ya unyang'anyi wa kutumia silaha katika Mahakama ya Rufani, iliyoketi jijini Arusha jana. **PICHA: ALLAN ISACK**

**MICHEZO** RUNGU LA TFF LAWAANGUKIA KIBU, DIARRA UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Hoja sita zambeba Sabaya kushinda kesi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Rufani iliyoketi Arusha, imetupilia mbali rufani namba 231/2023 ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) kwa kuridhia hukumu iliyotolewa na Mahakama Kuu Kanda ya Arusha kumwachia huru aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake wawili.

Mei 6, 2022, Mahakama Kuu Masjala ya Arusha chini ya Jaji Sedekia Kisanya, ilimwachia huru Ole Sabaya na wenzake baada ya kubaini dosari katika hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha ya kifungo cha miaka 30 jela.

Hukumu hiyo ilitolewa Oktoba 15, 2021 na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Arusha, Odira Amworo baada ya kumtia hatiani katika kesi ya jinai namba 105 ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Silvester Nyegu na Daniel Mbura. Walikuwa wanakabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi kwa kutumia silaha.

Novemba Mosi mwaka huu, mahakama hiyo chini ya majaji watatu, wakiongozwa na Jaji Jacobs Mwambegele, Ignas Kitusi na Leila Mgonya, walisikiliza hoja sita za waleta rufani (Jamhuri), kupianga hukumu ya Mahakama Kuu kumwachia huru Ole Sabaya na wenzake.

Akisoma uamuzi wa hukumu hiyo jana mahakamani huko, Naibu Msajili wa Mahakama ya Rufani, Abeesiza Kalegeya, alisema hukumu hiyo inatokana na hukumu ya kesi ya jinai iliyotolewa na Jaji Kisanya wa Mahakama Kuu Masjala ya Arusha.

Alisema Mahakama ya Rufani ya awali (Mahakama Kuu) ilitengua uamuzi wa Mahakama ya chini (Mahakama ya Hakimu Mkazi) na waleta rufani walikata rufani Mahakama ya Rufani wakipinga hukumu hiyo.

Naibu Msajili alisema awali waleta rufani waliwasilisha mahakamani huko hoja saba lakini wakati wa usikilizaji wa rufani hiyo zilikuwa hoja sita.

"Ni wazi kweli mahakama ya awali wakati wa usikilizaji wa shauri haikuzingatia usomaji wa maelezo ya awali, lakini inatibika kwa kifungu cha 378 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jina," alisema.

Naibu Msajili alisema kuwa mahakama hiyo inaamani wakati wa usikilizaji shauri, mleta rufani alikuwa na uwakilishi na alikuwa anajua haki zake.

Vilevile, alisema kwa suala kushindwa kupewa haki kwa mjibu rufani wa pili na tatu kumhoji maswali ya dodoso shahidi wa pili wa upande wa mashtaka, ulikuwa ni ukiukwaji wa sheria.

"Mahakama hii imekwenda kuangalia kama ushahidi uliotolewa umethibitisha makosa bila kuacha shaka ila baada ya kuondoa ushahidi wa shahidi wa pili wa mashtaka bado ushahidi wa mashahidi wengine umeshindwa kuthibitisha mashtaka," alisema.

Naibu Msajili alisema kwa mujibu wa hati ya mashtaka, wajibu rufani walikuwa wameshtakiwa kwa makosa matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

"Ushahidi ulioletwa mahakamani haungi mkono hati ya mashtaka kulingana na ushahidi ulioletwa na mashahidi mahakamani. Kwa kuwa mahakama imeona kuna kasoro kwenye kiasi halisi cha fedha kilichokuchuliwa dukani.

"Si kitu cha kawaida kwa wajibu rufani kutenda makosa hayo halafu wawachukue wahanga (waathirika) wanaodaiwa kupigwa na kuwapeleka kituo cha polisi," alisema.

Naibu Msajili alisema wanaona shaka, hakuna ushahidi wa kuthibisha shtaka la kwanza na tatu la unyang'anyi wa kutumia silaha kulingana na ushahidi uliowasilishwa mahakamani.

"Wanajaribu kuonesha kuwa kwa kosa la kwanza na tatu Mahakama ya awali ilifanya kubadilisha kosa la pili kutoka ujambazi wa kikundi kwenda kuwa kosa la unyang'anyi wa kutumia silaha.

"Kutokana na yote niliyotafsiri Mahakama imeona kosa la ujambazi wa kikundi na unyang'anyi wa kutumia silaha halijathibitishwa kulingana na ushahidi, hivyo uamuzi uliotolewa na Mahakama Kuu, mahakama hii haiwezi kubatilisha hukumu hiyo na inatupilia rufani hii," alisema.

**NJE YA MAHAKAMA**

Baada ya uamuzi huo wa Mahakama ya Rufani, nje ya ukumbi wa mahakama hiyo, Wakili wa Wajibu Rufani, Mosses Mahuna, alidai mahakama hiyo imesema kinagaubaga kuwa inakubaliana na uamuzi wa Mahakama ya Rufani ya awali kuwa shtaka la ujambazi kwa kutumia silaha halikuthibitika na la ujambazi wa kutumia kundi.

"Mahakama ya Rufani imemwachia huru Sabaya kwa sababu tofauti na zile zilizotolewa na Mahakama Kuu, na katika hoja ambayo imetaja ni kosa zima la ujambazi kwa kutumia silaha halijathibitika na hata kosa dogo la ujambazi wa kundi ambalo mahakama ya awali ilibadilisha kosa la unyang'anyi wa silaha kwenda kosa la ujambazi wa kundi.

"Mahakama ya Rufani imesema mahakama ya awali ilikosea kufanya hivyo na hata kosa hilo halikuweza kuthibitika kwa kuwa mahakama hii imesema hakuna ushahidi wa aina yoyote ambao umeweza kuthibitisha mashtaka," alisema.



Kiongozi wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe akinunua mihogo kutoka kwa mmoja wa wafanyabiashara katika soko la samaki katika Mji wa Muhambwe, mkoani Kigoma jana, alipowatembelea ili kujua changamoto zinazowakabili. Habari Uk. 4. **PICHA: ABDALLAH KHAMIS**

# Tanzania na Romania zaweka mkakati sekta za afya, elimu

**Na Romana Mallya**

TANZANIA na Romania zimekubaliana kuendeleza zaidi uhusiano baina ya nchi hizo ikiwa ni pamoja na kubadilishana uzoefu katika sekta ya kilimo ikiwamo usindikaji wa mazao na kukabiliana na majanga.

Katika mazungumzo baina ya Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Romania, Klaus Werner Iohannis, Ikulu jijini Dar es Salaam jana, wawili hao pia walizungumzia fursa zilizoko katika sekta za afya na utengenezaji wa dawa.

Rais Iohannis yupo Tanzania kwa ziara ya siku nne na leo atakwenda Zanzibar na kufanya mazungumzo na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi na kutembelea vivutio vya utalii ukiwamo Mji Mkongwe.

Marais hao walishuhudia utiaji saini hati mbili za makubaliano, moja ikihusu kukuza ushirikiano wa kiuchumi kisayansi na kiufundi katika sekta ya kilimo na mazingira na nyingine ni hati ya makubaliano kati ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Romania kwa ajili ya kushirikiana katika kukabiliana na maafa na misaada ya kimataifa ya kibinadamu.

Rais Samia alisema ushirikiano baina ya nchi hizo mbili ulianza Mei, 1969 baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Samia alisema wamekubaliana kuongeza wigo wa ufadhili wa masomo husani katika fani za udaktari na famasia ambapo Romania imekubali kutoa nafasi 10 za masomo kwa Watanzania.

Alisema Tanzania nayo imetoa nafasi tano za ufadhili kwa vijana wa Romania kusoma kwenye vyuo nchini watakavyovichagua ikiwa ni fursa ya kuchangia jitihada za serikali za kujengea uwezo, rasilimali watu na kuimarisha huduma katika sekta mbalimbali.

Pia alisema wamekubaliana kuongeza kiwango cha biashara ambacho kimekuwa cha chini licha ya kwamba nchi hizo mbili zina historia ndefu ya ushirikiano.

"Tunahitaji kutafuta njia za kuongeza kiwango cha biashara lakini pia, kushughulikia vikwazo kwa kuwaalika wafanyabiashara kutoka nchi hizi mbili kujadili namna ya kuboresha biashara," alisema.

Rais Samia alisema hiyo ni ziara ya kwanza ya mkuu wa nchi kutoka Romania kuzuru Tanzania tangu ushirikiano baina ya nchi hizo mbili uanze.

Kuhusu mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi wa COP28, 2023, Rais Samia alisema Tanzania inatarajia kuweka nguvu suala la nishati na nishati safi ya kupikia, hivyo amemuomba Rais Iohannis kuiunga mkono Tanzania.

Rais wa Romania alisema nchi yake inaandaa mkakati mpya wa ushirikiano na nchi za Afrika ikiwamo Tanzania.

Alisema maeneo mengine ambayo wamekubali kuyatilia mkazo zaidi ni kilimo na usalama wa mtandao.

"Tumebaini kuna maeneo ambayo yanafanana katika nchi hizi tumeona yapo ambayo tunaweza kushirikiana na kuchochea ushirikiano katika kilimo, ulinzi wa raia, teknolojia na usalama kimtandao," alisema.

Ziara ya Rais Iohannis imeandaliwa kimkakati ili kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia, kiuchumi na kiutamaduni wa Romania na Afrika.

Tanzania na Romania zimekuwa zikishirikiana katika biashara na uwekezaji. Bidhaa kuu za Tanzania zinazosafirishwa kwenda Romania ni sangara wa Nile, chai, tumbaku na parachichi wakati Tanzania inaagiza kutoka Romania bidhaa za mashine za umeme, matrekta, magari na vifaa vya matibabu.

Takwimu zinaonyesha kuwa mwaka 2021, Tanzania ilisafirisha bidhaa zenye thamani ya Dola milioni 4.26 kwenda Romania huku Romania ikisafirisha bidhaa zenye thamani ya Dola milioni 12.3 kwa Tanzania.

HABARI KITAIFA



Meneja Miradi Mwandamizi wa Benki ya NMB, Hellen Dalali akizungumza wakati wa mkutano wa kujadili masuluhisho asilia ya kupambana na mabadiliko ya tabia nchi yaliyojikita kwenye biashara ya hewa ukaa, jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Mwakilishi Mkaazi wa FAO, Nyabenyi Tito Tipo na Profesa Yues Hauss kutoka, Association for the Development of Protected Areas (ADAP). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watoto kuzaliwa kabla ya wakati mtihani mgumu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

ASILIMIA 20 hadi 25 ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati (njiti) kisha kupoteza maisha 'wanawapasua vichwa' wataalamu wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini (KCMC) kutafuta namna ya kukabiliana na vifo hivyo.

Kati ya Januari hadi Novemba mwaka huu, watoto njiti 461 wamezaliwa KCMC huku idadi ya waliopokewa kutoka maeneo mbalimbali ni watoto 1,356.

Jana Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, Prof. Gilleard Massenga, akizungumza wakati wa mapokezi ya vitanda vya kutunzia watoto waliozaliwa kabla ya wakati vilivyotolewa na Benki ya Maendeleo, alisema:

"Hili eneo la watoto njiti, yaani watoto wanaozaliwa kabla ya umri wao kufika wa kuzaliwa, ni eneo ambalo bado hatujafanya vizuri kama nchi na kama hospitali. Ni eneo ambalo kidogo linahitaji msukumo.

"Nitoe shukrani kwa wenzetu wa Benki ya Mendeleo kwa kutupatia vitanda tiba, ambavyo vitasaidia kupunguza vifo vya watoto hawa wachanga wanaozaliwa kabla ya muda wao.

"Hali halisi ilivyokuwa sasa hivi watoto wanaozaliwa kabla ya wakati wao kufika, nikiangalia takwimu za mwaka huu kuanzia Januari hadi sasa (Novemba), watoto njiti ambao wamezaliwa hapa KCMC ni watoto 461.

"Na tunavyofanya kutokana na utaalamu wetu asilimia 23 mpaka 25 bado hatuwezi kuokoa maisha yao. Kwahiyo, bado ni wengi ambao wanapoteza maisha. Tuseme mpaka asimilia 70 mpaka 75 tunaweza tukapambana nao, lakini wengine wanapoteza maisha."

Kwa mujibu wa Prof. Masenga, matatizo yanayochangia kupoteza maisha kwa watoto njiti ni pamoja na hali ya kuwa na joto la chini la mwili (Hypothemia).

Kabla ya makabidhiano hayo, Mkurugenzi wa Benki ya Maendeleo, Dk. Ibrahim Mwangalaba, alisema kati ya Sh. milioni 120 zilizokusanywa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kupitia Maendeleo Bank Marathon Februari 9 mwaka huu, Sh. milioni 60, zimetumika kununua vitanda kwa ajili ya kusaidia watoto wetu wanaozaliwa kabla ya wakati katika hospitali hiyo.

Kwa mujibu wa Dk. Mwangalaba, fedha nyingine Sh. milioni 60, zitatumika kukarabati majengo chakavu ya kituo kinachotunza watoto wenye usonji kilichoko Kurasini, Dar es Salaam. Kimepewa jina la Mtoni Diakonia.

"Sisi kama Maendeleo Benki tutaendelea kufanya kila lililo kwenye uwezo wetu kuhakikisha kwamba juhudi hizi kupitia Marathon zinadumishwa," alisisitiza Dk. Mwangalaba.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Jairy Khanga, ameeleza kuwa kwa mujibu wa utafiti uliofanyika wa viashiria vya afya, ambao Rais Samia Suluhu Hassan aliuzindua hivi karibuni, Tanzania imepunguza vifo vya watoto wachanga kutoka vifo 25 kati ya vizazi hai 1,000 hadi vifo 24 kati ya vizazi hai 1,000. Mkuu wa Idara ya Watoto na Daktari Bingwa wa Watoto KCMC, Dk. Aisia Shayo, alifafanua kuwa Hospitali ya KCMC, inapokea watoto waliozaliwa kabla ya wakati kwa idadi kubwa.

"Kwa mwaka jana, tulipokea watoto 1,356. Pia watoto hao asilimia chache, tuliwaruhusu kwenda nyumbani, ambao ni chini ya asilimia 50 kutokana na changamoto tulizokuwa nazo.

"Tunajitahidi kupubnguza vifo vyao na tumejitahidi kujielekeza kwa wenye uzito kati ya kilogramu moja, mpaka 1.5 kwa sababu hao unaweza kuwasaidia. Kwa wale chini ya kilogramu moja kamili inakuwa ni shida lakini bado tunajitahidi kuwasaidia," alisema.

**BENJAMIN MKAPA**

Jijini Dodoma, mwandishi wetu Renatha Msungu anaripoti kuwa asilimia 11 ya wanawake milioni mbili nchini hujifungua watoto kabla ya wakati kwa mwaka, huku sababu kubwa ikitajwa kuwa lishe duni.

Sababu zingine ni pamoja na ugonjwa wa kisukari, shinikizo la damu na maradhi mengine ambayo huwakumba wanawake.

Daktari Bingwa wa Watoto ambaye pia ni Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Watoto, Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamin Mkapa (BMH), Julieth Kabengula, alibainisha hayo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto Njiti Duniani.

Dk. Kabengula alitoa ushauri kwa jamii hususani wanawake kuandaa mwili kupokea mabadiliko ya ujauzito ili kuepuka kuzaa kabla ya wakati kutokana na hali hiyo.

Kuhusu watoto kuzaliwa utumbo ukiwa nje, bingwa huyo alisema hali hiyo inatokana na wanawake kuzaa katika umri mdogo kuanzia miaka 18 hadi 20 au kuzaa wakiwa na umri wa zaidi ya miaka 45.

Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Dk. Alphonce Chandika alisema wagonjwa ambao wamepata matibabu ya moyo kwa njia ya kufungua kifua na kutokufungua wameruhusiwa na wanaendelea vizuri.

Dk.Chandika alisema BMH alisema inaendelea kutoa matibabu ya moyo kwa wagonjwa na kusisitiza jamii iendelee kujitokeza kupata matibabu ya ugonjwa wa moyo katika hospitali hiyo.

# Moshi wa jenereta waua watatu kwa mchungaji

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WATU watatu wamefariki dunia na wengine watatu kunusurika baada ya kuvuta hewa chafu ya moshi wa jenereta wakati wakilifanyia usafi ndani ya karo nyumbani kwa Mchungaji wa Kanisa la EAGT Utemini.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Peter Majira, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema tukio hilo limetokea Novemba 13, mwaka huu nyumbani kwa mchungaji huyo, John Mafwimbo, katika eneo la Sabasaba, Manispaa ya Singida.

Majira aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Michael Zacharia (54) Mkazi wa Utemini, John Damson (28) wa VETA na Samweli Sinda (30) wa Kibaoni katika manispaa hiyo.

Aliwataja walionusurika kuwa ni Mswede Malume (30), Ally Muka (26) na Emmanuel Damson (36) wakazi wa eneo la VETA.

Kwa mujibu wa Kamanda Majira, majeruhi hao walipelekwa katika Hospitali ya Rufani Mandewa na kuruhusiwa baada ya kupatiwa matibabu, hali zao zinaendelea vizuri.

Kaimu Kamanda huyo alisema uchunguzi wa awali uliofanywa na Jeshi la Polisi umebaini kuwa vifo na madhara kwa majeruhi hao, vimetokana na kuvuta hewa chafu iliyotokana na jenereta hilo walilokuwa wamelitumbukiza ndani ya karo kutoa moshi mwingi.

Katika tukio jingine; jeshi hilo linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya aina ya mirungi kilo 13.

Majira aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Steven Ndege (24) na David Nelson (24), wakazi wa Mwanza.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa katika Hoteli ya Miami iliyopo Manispaa ya Singida baada ya polisi kupata taarifa kuwa walikuwa na dawa hizo kwa ajili ya kuzisafirisha kwenda mkoani Mwanza.

Alisema watuhumiwa hao wanaendelea kuhojiwa na upelelezi ukikamilika watafikishwa mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

"Jeshi la Polisi Mkoa wa Singida linatoa rai kwa wananchi kujishughulisha na shughuli halali ili kukipatia kipato halali na halitasita kumchukulia hatua kali mtu yeyote ambaye atatenda kinyume na sheria za nchi," alisema.

Vilevile amewataka wananchi kuchukua tahadhari katika kipindi hiki cha mvua zinazoendelea kunyesha kuhakikisha usalama wao wanapokuwa katika shughuli zao ili kuepuka maafa yanayoweza kutokea.

## TAARIFA KWA UMMA



**POLYCUP OKUMU RACHUONYO**

**HIKIWAKI INSURANCE BROKERS**, ambayo ni Kampuni ya udalali wa bima, yenye makao makuu yake Dar es Salaam, Tanzania inapenda kutoa taarifa kwa umma na kwa wateja wake wapendwa kuwa Bwana Polycup Okumu Rachuonyo, ambaye ni raia wa Kenya sio mfanyakazi wa Hikiwaki tena na kampuni haitohusika na shughuli, wala ubadhirifu wowote atakaousababisha kwa kutumia jina la kampuni.

**Kwa mawasiliano zaidi piga: +255621843561**.

BAA LA KISUKARI

# Kila sekunde 20, mguu unakatwa

**Na Romana Mallya**

WATAALAMU wa afya wamebainisha kuwa katika kila sekunde 20, mgonjwa wa kisukari anakatwa mguu duniani.

Kwa Tanzania, wataalamu hao wamebainisha kuwa katika kila wagonjwa 100 wa kisukari, kuna uwezekano wagonjwa watano hadi 10 kupoteza miguu kwa mwaka.

Hayo yalibainishwa jana na wataalamu wa afya katika mkutano ulioandaliwa na Chama cha Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA), kuhusu kisukari na changamoto zake uliokutanisha pia wagonjwa wa tatizo hilo jijini Dar es Salaam.

Mtaalamu wa Ugonjwa wa Kisukari, Hospitali ya Rufani Temeke, Dk. Boniface Mphumuhila, alisema mgonjwa wa kisukari hadi kufikia kupata kidonda na kukatwa mguu, hutokana na kushindwa kudhibiti hali yake.

Dk. Mphumuhila alisema sukari inapokuwa juu kwa muda mrefu,inaathiri mishipa ya fahamu na ya damu kutofanya kazi vizuri.

Pia alisema husababisha hata akivaa viatu vya kawaida, akitembea umbali mdogo kiatu kinamtafuna na kutengeneza kidonda.

Alisema kwa wale ambao hawawezi kusafisha vizuri miguu, ni kama nyumba, itakuwa na panya. Kisukari nacho hutafuna vidole wakati wamelala na kupata vidonda ambavyo ni shida kupona hata wanapopewa dawa na kwa sababu hiyo huoza na tiba rahisi huwa ni kukata kiungo kilichoathirika.

"Kidunia kila sekunde 20 kuna mtu mmoja anakatwa mguu mahali. Ukifanya hesabu kwa dakika tunapoteza miguu mitatu. Kwa maana hiyo, shida ya miguu imekuwa kubwa mno, tunatengeneza walemavu wengi na wategemezi wengi kutokana na kisukari cha miguu.

"Tunahitaji jamii ijue ili kutunza miguu na kujiepusha na tatizo la kupoteza viungo. Kisayansi kama mtu ameshapoteza mguu mmoja, ndani ya miaka mitano ijayo ana uwezekano mkubwa kupoteza mguu wa pili," alisema.

Alisema takwimu za Tanzania, kila wagonjwa 100 wa sukari kuna uwezekano wa wagonjwa watano mpaka 10 wakapoteza miguu kwa mwaka.

"Hivyo, tunashauri watu wavae viatu vinavyoweza kuwafaa kwa afya na wenye shughuli zinazohusiana na moto kujiepusha na ajali za moto," alisema.

Daktari Bingwa wa Magongwa ya Figo Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Onesmo Kisanga ambaye pia ni Rais wa Chama cha Wataalamu wa Figo Tanzania, alisema ugonjwa wa kisukari ndio unaoongoza duniani kuleta shida ya figo.



Upimaji wa Kisukari

Alisema utafiti uliofanyika nchini, unaonesha asilimia 44 kisukari ndicho kinaongoza shida ya figo, kwa maana waliopata shida ya figo, waliopandikizwa na wanaofanyiwa usafishaji wa damu.

"Muhimu ni kuzuia kwa kuwa ugonjwa huu una hatua tano. Hatua ya kwanza na ya pili ni mapema tunaweza kudhibiti magonjwa ya figo. Mtu akifika hatua ya nne na ya tano tunafika kwenye kusafisha damu au upandikizaji figo ambapo ni ghali.

"Tunaposema mtindo wa maisha ndio lengo kuu. Kupima mara kwa mara afya na vipimo vyenyewe si ghali, ni kupima kisukari chenyewe, uzito na mkojo.

"Tunatoa elimu watu wapime angalau mara moja kwa mwaka na wasitumie ovyo dawa za kutuliza maumivu, mfano diclopar, chakula kula kuzidi nayo inaleta tatizo," alisema.

Dk. Kisanga alisema miongoni mwa wanaosafisha damu Hospitali ya Muhimbili, ni vijana, ikimaanisha kuwa kwa umri wao hawajaweza kuzuia tatizo mapema.

"Kila siku wagonjwa wanaosafishwa damu Hospitali ya Muhimbili ni 200, wanaofika kila siku kwa ajili ya kuingia chumba cha upasuaji ni kati ya 40 na 50, wanaolazwa kwa magonjwa sugu ya figo ni zaidi ya 20 na wagonjwa mpaka 10 kwa magonjwa ya ghafla na ICU ni wengi," alisema.

Daktari Aneceth Muchunguzi anayeishi na kisukari cha aina ya kwanza zaidi ya miaka 10 tangu mwaka 2013, alisema jamii imekuwa haifahamu kuwapo kisukari kwa watoto na vijana na kusababisha kundi hilo kupoteza maisha kabla ya kugundulika.

Dk. Muchunguzi ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wanaoishi na kisukari aina ya kwanza Tanzania (YDYA), alisema kisukari cha aina hiyo kinapogundulika mapema, yapo matibabu na kijana akatimiza ndoto zake kama yeye.

"Kisukari cha aina ya kwanza hutokea mara nyingi unakuta kinga ya mtu inakosea na kushambulia kongosho halafu linashindwa kutengeneza kichocheo kinachoitwa insulin - inayodhibiti kiwango cha sukari na mtu kupata kisukari cha aina ya kwanza na matibabu yake ni kutumia insulin bandia kila siku kuidhibiti," alisema.

Alisema endapo mtu anamwona mtoto wake anapungua uzito haraka ndani ya muda mfupi, anakunywa maji sana na kuwa na kiu iliyopitiliza licha ya kunywa maji, lakini hatosheki, anakwenda haja ndogo mara kwa mara na usiku anaamka hadi mara nne, kuchoka, haoni vizuri au kichefuchefu apelekwe hospitalini kuangalia kama ana tatizo hilo.

Alisema takwimu za dunia zinaonesha kuna zaidi ya watu milioni 500 mpaka 600 wenye kisukari na kati yao, karibu milioni 10 wana kisukari aina ya kwanza.

Alisema katika ukanda huu, watoto wamekuwa hawagundulikі mapema, hivyo wao wanaendelea kutoa elimu.

Pia alisema wanachohitaji zaidi ni kusaidiwa kwenye vifaa tiba kwa kuwa insulin wanayoitumia kila siku ni ya gharama ambapo mtu anaweza kutumia mpaka Sh. milioni tatu kwa mwaka ili kupata matibabu sahihi.

Aliiomba serikali iingilie kati suala hilo kwa kuhakikisha matibabu yanapatikana kwa gharama nafuu au kuwa bure ili kuhakikisha afya zao zinakuwa imara.

Mkurugenzi Msaidizi wa Magonjwa Yasiyoambukiza Wizara ya Afya, Dk. Omary Ubuguyu, alisema wamekutana kutoa elimu kwa jamii kuhusu magonjwa ya kisukari kwa kuwa mwezi huu huadhimisha siku ya magonjwa yasiyoambukiza na kila mwkaa ifikapo Novemba 14, ni siku maalum ya kujenga uelewa kuhusu tatizo hilo.

"Timu ya chama cha kisukari Tanzania pamoja na wagonjwa na wataalamu wamekutana. Si wakati wote tunapata fursa ya kueleza wagonjwa kwa kina kuhusiana na ugonjwa na namna ya kudhibiti.

"Tunapopata fursa ya kuita baadhi ya wagonjwa na kuwaelimisha, wanapata fursa ya kwenda kuwafundisha wenzao ili wawe mabalozi wazuri," alisema.

Takwimu hizo zimetolewa ikiwa leo ni kilele cha Wiki ya Magonjwa Yasiyoambukiza, kisukari kikiwa miongoni mwa magonjwa hayo.

## Zitto: Kambi za wakimbizi zifunguliwe, tufanye biashara

**Na Julieth Mkireri,**
KIBONDO

CHAMA cha ACT Wazalendo kimemtaka Mkuu wa Kambi ya Wakimbizi Nduta iliyoko Kibondo mkoani Kigoma, kuifungua ili wananchi wa wilaya hiyo wafanye biashara na wakimbizi hao na kukuza uchumi kwa pamoja.

Kimesema kitendo cha kufungwa kambi za wakimbizi ni moja ya vikwazo vikubwa katika ukuaji uchumi na maendeleo katika maeneo ya Kibondo.

Akiwa ziarani kwenye Jimbo la Muhambwe, Wilaya ya Kibondo jana, Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe, alihutubia wananchi na kukumbusha kuwa mkoa huo umekuwa unapokea wakimbizi tangu mwaka 1972.

Alisema licha ya uwekezaji mkubwa wa jumuiya ya kimataifa uliofanya, watu wa Kigoma wamekuwa wanalalamika kuwa ukarimu wao hauwapi faida.

Zitto aliahidi kulibeba suala hilo la kufungwa kwa kambi hizo na kwenda nalo kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, ili lishughulikiwe haraka.

"Sera ya wakimbizi ni ileile inayotumika Nyarugusi Kasulu na Kibondo, sasa iweje Kasulu waruhusiwe Kibondo wafungiwe kama si hujuma? Mkuu wa Kambi Kibondo aache uchumi ushamiri, aache kufunga kambi," alisema.

Akizungumzia ubovu wa soko maarufu la samaki ambalo wafanyabiashara wengi wanauza bidhaa zao huko, Zitto alisema atatafuta wafadhili kwa ajili ya uboreshaji.

Alisema miundombinu yake ni mibovu na wakati wa mvua wafanyabiashara wanafanya shughuli zao katika mazingira magumu, lakini halmashauri iko kimya katika maboresho yake.

Katika mpango wa pili wa Kigoma Joint Program unaofadhiliwa na mashirika ya kimataifa chini ya Umoja wa Mataifa, alisema kumetenga Sh. bilioni 220 kutatua vikwazo vya maendeleo ya Kigoma bila ya kufungamanisha wakimbizi na uchumi wa Kibondo.

# Wahitimu TIA wapewa kibarua

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TAASISI ya Uhasibu Tanzania (TIA) imewataka wahitimu watakaopata ajira serikalini, kusaidia kupunguza matatizo ambayo yamekuwa yakiibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya TIA, Wakili Said Chiguma, alisema hayo jana wakati wa mahafali ya 21 ya taasisi hiyo, Kampasi ya Singida ambayo wahitimu 1,700 walitunukiwa vyeti baada ya kuhitimu fani za uhasibu, rasilimali watu, ununuzi wa umma na usimamizi wa biashara.

Alisema wahitimu watakaopata ajira wakajiepushe na vitendo ambavyo ni kinyume cha kanuni za maadili ya taaluma zao ambavyo vinaweza kuwasababisha kupoteza ajira, heshima na hata kufungwa jela.

"Kutokana na CAG ambavyo ameibua matatizo mbalimbali, ninyi mtakaopata ajira serikalini muende kupunguza au kutoa matatizo hayo na sio kuyatengeneza, " alisema.

Chiguma alisema wahitimu hao wanatakiwa kufahamu kuwa jamii na taifa kwa ujumla wanategemea kuona ujuzi walioupata unawapa fursa mbalimbali za kiuchumi, biashara na kutengeneza ajira ambazo zitawanufaisha jamii.

Alisema TIA imeendelea kuwa kinara katika kuwanoa wahitimu wake ambao wanafanya vizuri katika soko hususani mitihani ya Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Mahesabu (NBAA) na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) ambapo wahitimu wa TIA waliibuka katika nafasi ya tano bora kati ya vyuo na taasisi zaidi ya 20.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TIA, Prof. William Pallangyo, alisema kumekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaojiunga katika taasisi hiyo kila mwaka wa masomo kutokana na ubora wa elimu inayotolewa kwa sababu ya uwapo wa mitaala inayowajengea wanachuo wa ngazi zote msingi wa umahiri.

Alisema sababu nyingine ya ongezeko la wanafunzi ni utaratibu mzuri wa serikali wa kuwapangia vyuo moja kwa moja wahitimu wa kidato cha nne waliofaulu na kukidhi vigezo kupitia Ofisi ya Rais tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na ongezeko la mikopo kwa wanafunzi wa kozi za shahada.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, katika mahafali hayo, alisema serikali ina mpango wa kukuza diplomasia ya uchumi, hivyo mafunzo wanayopata wahitimu wa TIA yaendane na shabaha ya Rais Samia Suluhu Hassan.

# Sababu wanaume kuoa wake wengi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASILIMIA 15 ya wanawake walioolewa wana mke mwenza mmoja au zaidi huku asilimia sita ya wanaume wakiwa na wake wawili au zaidi nchini, takwimu rasmi za serikali zinabainisha.

Viongozi wa dini wametaja sababu zinazochangia hali hiyo. Miongoni mwa sababu hizo ni utandawazi, wanawake kukosa utii kwa waume zao na wanaume kupenda unafuu wa maisha kwa kukubali kulelewa.

Askofu wa Kanisa la Covenant Faith Church Pentekoste, Damas Thadey, alimwambia mwandishi wa habari hizi jana kuwa kuongezeka kwa uke wenza nchini kunachangiwa pia na wanaume kupenda unafuu wa maisha na kushindwa kutimiza wajibu wao.

"Unakuta mtu ana ndoa yake, lakini kutokana na ugumu wa maisha mwanamume anatumia utu wake vibaya kwa kutaka kulelewa na mwanamke.

"Kwahiyo, anakuwa na familia lakini pia analelewa na mwanamke mwingine. Ninyi vijana mnawaita 'marioo'," alifafanua.

Kiongozi huyo wa kiroho aliendelea kufafanua kuwa kwa sasa ndoa imeshushwa thamani kiasi ambacho watu wanaweza kufunga na kuachana kirahisi tofauti na miaka ya nyuma.

"Hizi ndizo zile nyakati za mwisho tulikuwa tukielezwa kuwa kuna vitu vya ajabu vitatokea. Ni pamoja na wanaume kutaka kulelewa na wanawake badala kutimiza maagizo ya Mungu kama mume anavyotakiwa kufanya katika ndoa yake," alionya.

Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, alisema sababu nyingine zinazochangia wanaume kuoa wake wengi ni kukosa hofu ya Mungu, pia wanawake kukosa utii kwa waume zao kama ambavyo maagizo ya dini yanafundisha.

Alisema kwa mujibu wa dini ya Kiislamu, suala la uke wenza limewekwa ili kupunguza zinaa na mwanamume wa Kiislamu amepewa rukhsa kuoa wake hadi wanne.

"Kama wanaume hawa wenye wake wangezuiliwa kuoa wake wengine, unafikiri hawa wengine wangepata wapi haki zao? Kwahiyo, ndoa ya uke wenza imewekwa mahususi kwa ajili ya shida hiyo na wanawake wanapaswa kuelewa," alisema

Shekhe Rajabu pia alisema ndoa za aina hiyo zimeongezeka nchini kwa kuwa ni sehemu ya maandiko ambayo yameandikwa katika vitabu vya dini kuwa wakati wa kiama kutashuhudiwa kukithiri kwa ulevi na zinaa.

"Hii pia inaweza kuwa moja kati ya sababu ambazo zipo katika vitabu vya dini kuwa wakati wa kiama kutakuwapo na kukithiri kwa mambo mengi ya ajabu kama vile ulevi na hivi sasa unaona ambavyo watu wamekuwa walevi, lakini pia zinaa. Watu wanaoana na kuolewa bila hata kufuata taratibu," alionya.

Alisema utandawazi pia umekuwa chanzo kikubwa cha ndoa za uke wenza kutokana na kujifunza mambo ambayo si mila na desturi.

Kwa mujibu ripoti ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022 (DHS-MIS 2022) iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na Wizara za Afya, asilimia 15 ya wanawake walioolewa wana mke mwenza mmoja au zaidi huku asilimia sita ya wanaume nchini (walio katika umri wa kuoa) wana wake wawili au zaidi.

Ripoti hiyo pia inaonesha kuwa ndoa za mitala zipo zaidi kwa wanawake na wanaume ambao hawana elimu na wanaoishi katika kaya maskini.




Meneja Mwandamizi wa Biashara wa Benki ya Mwanga Hakika, Judith Halinga (wa pili kushoto), akizungumza kabla ya uzinduzi wa akaunti ya pinki na kadi ya pink, jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Ofisa Mtendaji Mkuu Kampuni ya JSG Travellers, Venancia Msita (kushoto), Mteja wa benki hiyo, Graciana Mgeni (kulia) na Mwanasaikolojia, Sadaka Saidi maarufu kama Anti Sadaka. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Benki kuwezesha wanawake kutimiza malengo kifedha

**Na Joseph Mwendapole**

BENKI ya Mwanga Hakika imekuja na huduma ya Pinki Mwanamke Account ambayo itawawezesha wateja wanawake kuweka akiba huku wakipata faida mbalimbali ikiwamo kupata faida ya kwenye amana zao.

Akaunti hiyo ni rafiki kwa wanawake wa aina zote na ni mahususi kwa wanawake wenye ndoto za muda mfupi na mrefu na itawawezesha kuyafikia malengo hayo bila kutumia nguvu kubwa.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo jana, Meneja wa Biashara wa Benki hiyo, Judith Halinga, alisema wamekuwa mstari wa mbele katika kusogeza huduma za kibenki karibu na wateja ili kuboresha maisha ya Watanzania.

"Benki yetu tangu ilipopata hadhi ya kuwa benki rasmi ya biashara, tumekuwa mstari wa mbele kuendeleza ajenda ya ujumuishwaji wa watu kiuchumi kwa kuja na huduma za kibunifu zinazokidhi mahitaji ya kifedha," alisema.

"Hii inathibitika leo ambapo tunazindua Pinki Mwanamke Account ambayo itaboresha huduma za kibenki kwenye soko. Kwa kupitia akaunti hii, wanawake nchini bila kujali kipato chao wanapata fursa ya kuhifadhi fedha zao kwa uhakika zaidi huku amana zao zikiwasaidia kupata faida mbali na kutunza fedha," aliongeza.

Huduma hiyo imekuja wakati Watanzania wengi wamekuwa na mwamko mkubwa wa kufuatilia matumizi yao ya fedha. Kwa mujibu wa ripoti ya utafiti wa Fin Scope ya mwaka 2023, asilimia 77 ya Watanzania wanafuatilia matumizi ya pesa zao.

Hiyo ina maana kwamba uelewa juu ya umuhimu wa kuwa na taarifa za mapato na matumizi umeongezeka hivyo ni muhimu kwa taasisi kuja na suluhu za kifedha zitakazowasaidia kufanikisha malengo yao.

Huduma hiyo inakuja na manufaa mbalimbali kama kufungua akaunti bure, hakuna makato ya mwezi na riba itakokotolewa na kulipwa kila mwezi.

Pia akaunti hiyo itawawezesha wateja kupata mikopo bila riba ambayo itawasaidia kufanikisha malengo ya muda mfupi bila kuharibu au kugusa amana zao.

"Kama benki inayokua kwa kasi, tumeenda mbali zaidi na kuja na suluhu ambayo itakidhi mahitaji ya watanzania wengi zaidi.Tunaamini kwamba kupitia akaunti hii watanzania wengi zaidi bila kujali kipato chao watakuwa na uwezo wa kupatan huduma za kibenki na kufungua milango ya mafanikio," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Jagjit Singh.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Taifa Stars ni ya kwetu, tuiunge mkono, tuipende

**LEO** timu yetu ya taifa 'Taifa Stars' ina kibarua kigumu cha kusaka ushindi kwenye mchezo wa kuwania tiketi ya kufuzu fainali za kombe la Dunia za mwaka 2026.

Taifa Stars inayonolewa na Kocha Adel Amrouche itaumana na Niger ambao wamechagua kucheza mchezo huo nchini Morocco.

Baada ya mchezo huo, Taifa Stars itarejea nchini haraka kwa ajili ya kuikabili timu ya taifa ya Morocco kwenye michuano hiyo ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Dunia ambalo Taifa Stars haijawahi kushiriki.

Kwa namna ya ratiba ya mechi hizi ilivyo, ni wazi Taifa Stars ina kibarua kigumu katika kipindi cha wiki moja kwa sababu baada ya mchezo wa leo, Stars itarejea nchini kujiandaa na mchezo mwingine Jumanne ijayo kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kimsingi timu yetu inahitaji sapoti kubwa kutoka kwetu Watanzania, kila mpenda soka katika nchi hii anashauku kubwa ya kuona Taifa Stars siku moja inashiriki fainali za Kombe la Dunia, hiki ni kitu kinachowezekana kama kutakuwa na mikakati mizuri.

Ikumbukwe, Taifa Stars ilikaa kwa zaidi ya miaka 30 bila kushiriki fainali za Afrika tangu ilipofanya hivyo mara ya mwisho mwaka 1980 enzi za akina Leodgar Tenga ambaye baadaye alikuja kuwa rais wa Shirikisho la soka Tanzania (TFF).

Kama tuliweza kufanya hivyo, ni wazi hata kufuzu kwa fainali za Kombe la Dunia inawezekana kama watanzania kama nchi tutaungana pamoja kuisapoti timu yetu huku pia kwa viongozi kuweka mikakati mizuri na endelevu ya kuhakikisha tunafuzu fainali hizo.

Taifa Stars ni timu yetu, hakuna mtu wa nje ya nchi hii atakayekuja kuipenda na kusapoti taifa Stars kuliko sisi wenyewe wamiliki wa timu.

Sasa basi, leo taifa Stars inacheza ugenini nchini Morocco, ni wai watanzania wengi hawatakuwepo uwanjani na wataangalia mchezo huu kupitia Luninga, sasa basi kazi yetu iwe kwenye maombi kuhakikisha Taifa Stars inafanya vizuri.

Wakati Taifa Stars wakicheza leo, tuweke kwenye ratiba zetu kuwa itacheza mchezo wake wa pili Jumanne ijayo kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa, hapa ni vizuri mashabiki, na wananchi wapenda mpira na mapenzi mema kwa timu yetu kujitokeza kwa ingi uwanjani kuwapa sapoti wachezaji wetu.

Taifa Stars ikishinda katika ramani ya soka inatajwa Tanzania kufanya vizuri, na Tanzania ni sisi wananchi wenyewe, kwa nini tusiipende timu yetu na kuisapoti ili ituletee sifa.

Watanzania tunaweza kwa sababu wengi ni wapenzi wa soka, mahabana sapoti tunazozitoa kwenye klabu zetu hususani klabu kubwa za Simba na Yanga sasa tuzihamishie kwenye timu yetu ya taifa.

Taifa Stars ni timu inayokusanya wachezaji kutoka katika klabu mbalimbali za hapa nchini, humo ndani kuna wachezaji wa Simba, Yanga, Azam na nyingine hivyo ndio sehemu pekee mashabiki wa timu zote kuunganisha hisia zetu na mapenzi kwenye kitu kimoja.

Kwenye mpira hakuna kitu kisichowezekana ndani ya dakika tisini uwanjani pasipo kuangalia nani unacheza naye, iwe timu kubwa yenye rekodi nzuri au timu ya kawaida, lolote linawezekana.

Hakuna haja ya kuogopa majina makubwa ya nchi katika soka la Afrika, kila kitu kinawezekana, kikubwa ni kujua wajibu na juhudi za wachezaji wetu katika kile tunachokipigania.

Tujitokeze kwa wingi uwanja wa Benjamin Mkapa siku ya Jumanne kuipa sapoti timu yetu iweze kupata ushindi ambao utaendelea kuweka hai harakati zetu za kufuzu fainali za zijazo za Kombe la Dunia

Nipashe kama mdau mkubwa wa soka, tunaitakia kila la heri Taifa Stars katika kampeni ya kufuzu fainali za Kombe la dunia, tunaamini hakuna kinachoshindikana kwenye soka, Taifa Stars ni timu yetu na lazima tuipende na kusapoti.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Viongozi Simba, mtoto umleavyo ndivyo akuavyo

Na Adam Fungamwango

**VIONGOZI** wa Simba wanawatuhumu baadhi ya wachezaji wa timu hiyo kuwa walichukua rushwa ili kuihujumu kwenye mechi yao dhidi ya Yanga na kusababisha kupata kipigo cha mabao 5-1 Novemba 5, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Baada ya wao wenyewe kujidhihirishia kuwa kuna viashiria hivyo, wamepeleka majina ya wachezaji wanaowatuhumu kwenye Kamati yao ya Maadili inayoongozwa na Kamanda wa zamani wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam Kamishna Suleiman Kova.

Mara nyingi kwa uzoefu wangu kwenye michezo, tuhuma nyingi za kuhujumu timu huwa ni kwa upande wa klabu za Simba na Yanga.

Mara chache sana tunasikia kwenye timu nyingine sijawahi kusikia kitu kama hicho kwa timu katika ligi za Ulaya kama England, Hispania au Ujerumani, lakini huku upande wa Simba kumekuwa na tuhuma hizi mara kwa mara. Kwa nini?

Imekuwa ni rahisi kwa wachezaji wa Simba kuhujumu timu kwa sababu kwa miaka mingi viongozi wanapingana katika klabu hiyo, wamekuwa wakiwatumia kufungisha ili kutengeneza migogoro fulani ili kiongozi mlengwa aonekane hajui kuongoza.

Tangu miaka ya 1980, kulivyokuwa na mgogoro uliofanya kunusurika kushuka daraja chini ya Katibu Mkuu, Jimmy Ngonya, baadhi ya viongozi wa Simba walikuwa na tabia ya kuwapigisha shoti wenzao kwa kuwatumia wachezaji ili wanachama na mashabiki wawaone hawajui kuongoza na kuwaondoa madarakani.

Hii pia ilisikika miaka ya 1990, upande wa uongozi na kundi maarufu la Friends of Simba.

Waswahili wanasema ndugu mkigombana au kuuana wenyewe kwa wenyewe, hata majirani watanatumia mbinu hiyo kuwamaliza.

Kujituma nako kumekuwa tatizo kwa wachezaji wa Simba kwa muda mrefu, wamekuwa wakicheza kigoigoi tofauti na wapinzani wao wakubwa Yanga.

Simba hata ikiwa na wachezaji bora wa daraja la juu, huwa wanacheza kibishoo zaidi na Yanga hata ikiwa na wachezaji wa kiwango cha chini au cha juu mara nyingi hucheza kwa kujituma sasa.

Ndiyo maana haikushangaza hata Simba bora kabisa ya kuanzia mwaka 2017 pamoja na kufanya vyema kimataifa, lakini ilikuwa ikifungwa mara nyingi na Yanga ambayo ilikuwa ikitolewa kwenye mechi za awali tu za Ligi ya Mabingwa, ikiwa na wachezaji wa kawaida tu.

Hivi karibuni, Rais wa Yanga, Injinia Hersi Said aliwaambia wachezaji wake kinagaubaga kuwa hawatomvumilia mchezaji ambaye hatojituma, dirisha dogo litamhusu.

Ni kauli ya kishujaa na ya kiuongozi, na hii ndiyo inasababisha mchezaji kujituma, kwani analipwa pesa nyingi, na wale wa nje wanalipiwa kila kitu, mshahara, posho, vibali vya kufanya kazi na vya kuishi nchini, lakini anachezaje kama amelazimishwa?

Kauli hiyo ndiyo inasababisha wachezaji wa Yanga wanapambana kana kwamba wanacheza mechi ya mwisho kwenye dunia hii.

Upande wa Simba viongozi wake wamekuwa laini sana kwa wachezaji, wakati wanachama na mashabiki wanalalamika kuwa wachezaji hawajitoi ipasavyo zaidi ya Kibu Denis, viongozi wake wamekuwa kimya.

Hawakukaa na wachezaji kuwaambia ukweli, wakawaacha mashabiki wao wanapiga kelele.

Lakini baada ya kipigo kikali cha mabao 5-1, kilichosababisha wanachama na mashabiki kuchachamaa wakiwataka viongozi wajiuzulu, ndipo walipojitokeza na kudai wachezaji wao hawajitumi.

Ndiyo sasa nimesikia Mwenyekiti wa Bodi ya Simba, Salum Abdallah 'Try Again' akitoa povu kuwaambia wachezaji asiyejituma Januari anaondoka.

Siku zote mchelea mwana kulia, hulia yeye, na mtoto umleavyo ndivyo akuavyo, viongozi Simba kwa muda mrefu wamewalea 'kimayai' na kirafiki zaidi wachezaji wao, matokeo yake wamekuwa wanacheza kana kwamba wanajitolea tu kuisaidia timu na hawalipwi.

**MAKALA**

# Serikali yakunwa uwekezaji kiwanda TPC

**Na Mwandishi Wetu**



Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu (kulia), akijadiliana jambo na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kiwanda cha Sukari cha TPC, Marius Jacobs, baada ya mkutano mkuu wa wanahisa wa TPC uliofanyika juzi, mkoani Kilimanjaro. **PICHA: TRO**

"SISI wawekezaji tumefurahi na kuridhishwa na ufanisi katika uendeshaji wa kiwanda hiki cha sukari cha TPC Limited. Ufanisi huu unatokana na faida iliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2022/23. Kiwanda kimezalisha faida baada ya kodi ya Sh. bilioni 72.7 kutoka katika mauzo ya Sh. bilioni 235 huku gawio kwa wanahisa likiwa Sh. bilioni 69.9."

Hiyo ilikuwa kauli ya Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, baada ya kikao cha wanahisa kilichofanyika juzi mkoani Kilimanjaro, akielezea matokeo chanya ya uwekezaji katika kiwanda hicho.

Tangu mwaka 2000, Mchechu anasema kiwanda kimekuwa kikiongeza uzalishaji mwaka hadi mwaka na sasa uzalishaji umeongezeka kutoka tani 36,000 mwaka 2000 hadi kufikia tani 116,700 kwa mwaka huu.

Ongezeko hilo, kwa mujibu wa Mchechu, limetokana na ongezeko la mavuno ya miwa baada ya mwaka huu kuvunwa zaidi ya tani 1,150,000.

"Katika uzalishaji wa sukari kwa mwaka huu, TPC Limited imezalisha zaidi ya tani 116,700 katika kipindi cha Juni, 2022 hadi Machi, mwaka huu.

Hiki ni kiwango kikubwa cha sukari ambacho hakijawahi kuzalishwa katika miaka yote tangu TPC Limited kuanza uzalishaji mwaka 1936," anabainisha Mchechu.

Msajili anabainisha zaidi kuwa wakati ubinafsishaji wa kiwanda hicho unafanyika, serikali ilikuwa imeweka malengo shamba la TPC baada ya kuongezewa eneo la shamba la Kahe, itazalisha tani 750,000 kwa mwaka, lakini kwa sasa uzalishaji umefikia tani 1,150,000 kiwango ambacho ni juu ya malengo yaliyokuwa yamewekwa.

"Eneo lile lile lakini uzalishaji unazidi kuwa mkubwa kutokana na tija katika uzalishaji.

Kwa mwaka huu, TPC imetoa tija ya wastani wa tani 148 kwa hekta, kiwango ambacho ni cha juu barani Afrika. Hiki ni moja kati ya viwango bora vitatu duniani," anasisitiza.

Kuhusu sababu za ufanisi na mafanikio hayo, Mchechu anasema serikali ya sasa iliyoko madarakani chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, imeweka nguvu na jitihada kubwa za kuhamasisha kilimo na kuvutia uwekezaji katika kilimo hususani katika sekta ya sukari na hilo limefungua fursa nyingi za uzalishaji wa bidhaa hiyo nchini.

Anasema mambo ambayo yamefanyika katika kipindi cha serikali ya sasa ni pamoja na kuendelea kulinda soko la ndani dhidi ya sukari zinazoingizwa zenye kiwango cha chini na kuja kushindana na sukari inayozalishwa nchini yenye kiwango bora.

Kitendo hicho, anasema kimefanya sukari kuendelea kuuzwa katika bei nzuri, hivyo kuhamasisha wazalishaji wa sukari kuendelea kuwekeza zaidi katika soko la sukari.

"Tumeshuhudia serikali imekuwa na mfumo unaoeleweka na endelevu wa uagizaji sukari kutoka nje ya nchi.

Hii ni kutokana na maboresho yaliyofanyika katika sheria ya sukari pamoja na kanuni zake ambapo uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi, umewekewa utaratibu mzuri zaidi," anasema.

Mchechu anataja eneo lingine ambalo serikali imefanya ni kuhamasisha na kuhakikishia wawekezaji mazingira mazuri ya uwekezaji.

Anasema hali ambayo imechangia kuongezeka kwa wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi wanaowekeza katika sekta ya sukari.

"Viko viwanda mbavyo vimeanza kufanya kazi lakini pia kuna viwanda vingine vinakuja kuongeza uzalishaji wa sukari nchini. Katika mazingira haya tumeona serikali imesukuma mbele jitihada za kukuza kilimo hususani cha miwa ili kuongeza uzalishaji wa sukari nchini," anasema.

Katika kuunga mkono jitihada hizo za serikali, anasema TPC kwa mwaka huu wanatarajia kuwekeza fedha Dola milioni 45 hadi 50 kwa kujenga kiwanda kipya cha kuchakata molasses ambayo imekuwa ikibaki baada ya uzalishaji wa sukari.

"Bodi yetu leo itaidhinisha matumizi ya zaidi ya Dola milioni 45 au milioni 50 kwa ajili kuweka kiwanda kingine cha uchakataji molasses na kuzalisha bidhaa nyingine ambayo itakuwa 'spirit' kwa ajili ya matumizi ya viwanda na watumiaji wengine," anasema.

Kwa mujibu wa Mchechu, kiwanda hicho kitajengwa TPC na ujenzi unatarajiwa kuanza mapema mwakani na kwamba hicho ni kiwango kikubwa cha fedha kitakachowekezwa ikiwamo kukuza uzalishaji wa miwa na bidhaa zinazotokana na zao hilo.

Uwekezaji huo kwa TPC, anasema utakuza ajira na kuongeza mapato ya ndani ya kiwanda na kuwezesha kulipa kodi nyingi zaidi na manufaa mengine yatakayopatikana.

Kubwa zaidi, anasema kutakuwa na ongezeko la uzalishaji umeme na kwamba katika kiwanda hicho wanatarajia kufunga mashine nyingine ya kuzalisha umeme,. Kwa kufanya hivyo, anasema kutakuwa na ziada ya megawati nne hadi saba ambazo zitaingizwa katika gridi ya taifa.

**MCHANGO WA KIWANDA**

Kuhusu mchango wa TPC kwa jamii, Meneja Utawala wa kiwanda hicho, Jafary Ally, anasema kampuni imelipa kodi, ushuru na gawio kwa serikali ambazo ni zaidi ya Sh. bilioni 99 .

Ally anasema kiiwango hicho ni kikubwa kulinganisha na Sh. bilioni mbili kiasi kilichokuwa kikitolewa wakati kampuni hiyo imebinafsishwa mwaka 2000.

Anataja sababu kubwa ya kuongezeka kwa kiwango hicho ni uzalishaji, mauzo mazuri na ulipaji sahihi wa kodi kwa mujibu wa sheria na miongozo iliyowekwa.

"Mwaka 2010 kiwanda kilianza kulipa gawio serikalini na hadi mwaka 2022/23 tumekuwa tukilipa gawio na kiwango kimekuwa kikiongezeka mwaka hadi mwaka, hivyo kuifanya TPC kuongoza kwa miaka mitatu mfululizo kwa kutoa gawio zuri na kubwa serikalini kuliko mashirika mengine yote ambayo serikali ina hisa kidogo," anasema.

Akizungumzia mchango wa kiwanda hicho kwa jamii, Ally anasema kupitia shirika lisilo la kiserikali la FTK, wamekuwa wakitumia Sh bilioni 1.2 kwa mwaka kwa ajili ya kuhudumia jamii ya vijiji vinavyowazunguka. Fedha hiyo inaelekezwa kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta za elimu, afya, miundombinu na miradi endelevu ya vijiji kama vile umwagiliaji.

"Kwa upande wa utoaji wa huduma katika vijiji vinavyotuzunguka, tumeendelea kuboresha huduma. Kwa upande wa elimu, hivi karibuni tumejenga shule ya sekondari ya Chekereni/Weruweru (CHEWE) ambayo ni ya serikali.

Serikali ilituletea fedha za UVIKO - 19 zikaja kuongezea majengo ambayo yamefanya shule kuwa na vitu vingi vilivyokamilika.

"Ni shule inayoanza lakini ina vitu vyote muhimu ikiwemo madarasa, vyoo, jiko, madawati, maabara zote pamoja na jengo la utawala na shule hii itazinduliwa hivi karibuni baada ya serikali kukamilisha uwekaji wa samani," anasema.

"Lakini pia tumetoa huduma za afya na kujenga miundombinu ya barabara kutokana na uwezo tunaokuwa nao ikiwa ni pamoja na kuchimba visima na kujenga mabwawa ya kuoshea mifugo katika vijiji vinavyotuzunguka," anaongeza.



# BRELA yatoa angalizo katika kumiliki hisa kwa wanandoa

**Na Romana Mallya**

OFISA Mtendaji Mkuu Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Godfrey Nyaisa, amewafunda wajasiriamali wanawake kuhakikisha wanapokuwa na umiliki wa hisa katika kampuni, wafuatilie BRELA ili kujiridhisha kwa kuwa kundi hilo ndilo huumizwa zaidi.

Vilevile, amewataka wasajili bidhaa zao wanazoanzisha ili kuepuka mtu mwingine kufanya hivyo kwa jina la vitu wanavyozalisha na kuingia kwenye migogoro ya kisheria.

Nyaisa aliyasema hayo juzi mkoani Dar es Salaam wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Ujasiriamali Duniani iliyoandaliwa na Programu ya Women Creating Wealth iliyo chini ya Taasisi ya kimataifa ya Graca Machel Trust inayofanya kazi katika nchi mbalimbali.

Alisema changamoto ambazo ofisi yake imekuwa inakabiliana nazo ni zinazohusu umiliki wa hisa katika kampuni na usajili wa bidhaa huku akiweka wazi kuwa wanawake ndio waathirika zaidi.

Katika maadhimisho hayo yaliyohusisha wanawake wajasiriamali, Nyaisa alisema wanawake wana changamoto nyingi kwenye umiliki wa hisa za kampuni wanazozianzisha au zilizoanzishwa na wenza wao.

Aliweka wazi kuwa wanaweza kuambiwa na wenza wao kuwa ni sehemu ya wanahisa bila ya kwenda BRELA kuhakikisha hilo.

"Na wanawake mkipenda, mnapenda kweli, hivyo unaamini kwamba 'mume wangu kaniweka humo', sasa mume anafariki dunia au ni mwanahisa kampuni nyingi hujui.

"Kiutaratibu mume wako anapofariki dunia kama alikuwa na umiliki wa hisa katika kampuni fulani wale waliobaki lazima watoe taarifa. "Tukiwaambia tuleteeni cheti cha kifo, wengi wanachofanya wanabadilisha tu, haleti taarifa kwa kuwa anajua akileta taarifa tutamtaka atupatie muhktasari wa kikao cha familia, sasa anazunguka," alisema.

Nyaisa alibainisha wapo wengine wanafika katika ofisi hizo kwa maaelezo kuwa ameambiwa mume wake amemtoa katika umiliki wa hisa na akiangalia ni kweli.

"Sasa unamwuliza 'je, hii ni saini yako, anakiri ni yake, ukimwuliza ilikuaje umejitoa kwenye kampuni?' Atakwambia 'siku hiyo nilikuwa ninanyonyesha, mume wangu akaja akaniambia, karatasi inatakiwa BRELA saini haraka, nikasaini', amesaini kumbe amejiondoa," alisema.

Kiongozi huyo alitoa mfano mwingine wanaokutana nao ni baadhi ya wanawake wanakuwa na kampuni, lakini katika mchakato mwanamume anajiweka kuwa na umiliki wa hisa nyingi bila mwanamke kujua. "Unaanzisha kampuni unachofuatilia ni kama imesajiliwa. Kuna mtu kaja yeye ni mwanasheria amejiweka kama mmoja wa wanahisa wa kampuni.

"Kwenye ndoa ndio vita pekee ambayo maadui wanalala kitanda kimoja. Wapo ambao wapo vizuri lakini kwa kiasi kikubwa mtu anafariki dunia, inakuja kutuletea changamoto pale, kuna watu wakubwa, matajiri wakubwa wamefariki dunia wana mgogoro pale kwangu," alisema.

Alitolea mfano mwingine wa mtu ambaye wakati watoto wake wakiwa wadogo, aliamua kumwandika mdogo wake kama mwanahisa katika kampuni yake, lakini baadaye watoto walipofikia umri wa miaka 18, alipotaka kumwondoa ndugu yake akagoma.

"Tukiwa hai shemeji zetu, baba wadogo unaona wamekaa sebuleni, akiondoka (mwenzako) wanabadilika na kuwa wanyama na ndizo kesi tulizonazo pale. Wekeni vitu vyenu sawa mapema.

"Mfano mtu amefariki dunia na walikuwa wanahisa wawili ndani ya kampuni, mke wake hakuwahi kujua alikuwa anasikia tu, yule mwingine (baada ya mwenzake kufariki) akabadilisha nyaraka akamwingiza mke wake. Tulipoangalia kwenye faili ni kama marehemu alifufuka na kuhamisha hisa zake alafu akafa tena," alisema.

Alitaja eneo lingine lenye changamoto ni mtu anaanzisha bidhaa yake, lakini haisajili, hivyo kutoa mwanya kwa mtu mwingine kuzalisha vitu vilevile ambavyo mwanzilishi wake yupo.

"Sisi tunatetea mtu aliyesajili, hatutetei mtu ambaye anakimbia kodi. Kama una bidhaa unazotengeneza, njooni BRELA, tuna wataalamu watawasaidia kitaalamu msajili bidhaa zenu, sasa hivi kila kitu kinafanyika mtandaoni.

"Watu wengine ni wajanja wakiona jina limekua wanakuja BRELA anaangalia akiona halijasajiliwa analisajili halafu anapotea, siku ukisajili anakupeleka mahakamani, umesajili jina lake," alisema.

Alihamasisha wanawake washirikiane na BRELA kwa kuwa bila kufanya hivyo wataendelea kudhulumiwa.

Katika hotuba ya Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe iliyosomwa kwa niaba yake na Nyaisa, alisema serikali imekuwa inasisitiza kuhusu kuwawezesha Watanzania wakiwamo wanawake huku ikiweka mazingira ya kuzaidia wajasiriamali.

Meneja wa Programu ya Women Creating Wealth (WCW) ambayo ipo chini ya Graca Machel Trust , Anabahati Mlay, alisema imejikita kuwajengea uwezo wanawake wajasiriamali kukuza biashara zao na kuwa za kudumu na zinazotengeneza mali.

Alisema mkutano huo umeandaliwa Tanzania kama moja ya nchi zinazofanya programu hiyo iliyoanza nchini tangu mwaka 2017.

"Kwa mwaka huu tumeamua kuendana na Wiki ya Ujasirimali Duniani iliyoanza Jumatatu ya wiki hii na inaisha Ijumaa (jana).

"Tumejadiliana ni kwa namna gani tunaweza kushirikiana kuhakikisha wanawake wajasiriamali wanatoka katika biashara ndogo na kutengeneza biashara zenye faida," alisema.

# Ahukumiwa kunyongwa kwa kuua watoto watatu wa baba yake mdogo

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Iringa iliyofanya kikao chake mkoani Njombe, imemuhukumu Joel Nziku kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kuwaua watoto watatu wa familia moja, wote watoto wa baba yake mdogo.

Kesi hiyo namba 108 ya mwaka 2021 imesimamiwa na Mawakili wa Serikali, Pienzie Nichombe, Magdalena Whero na Wakili Mwandamizi wa Serikali, Dhamiri Masinde. Upande wa utetezi umesimamiwa na Alex Mgani.

Akisoma hukumu hiyo, Jaji Abubakari Mrisha alisema mshtakiwa Joel Nziku alitekeleza mauaji hayo mwezi Januari mwaka 2019 katika Kijiji cha Ikando, Kata ya Kichiwa, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Jaji Mrisha alisema mshtakiwa alikwenda nyumbani kwa baba yake mdogo na kuwachukua watoto watatu ambao aliwapakia katika lori, baadaye akawaua kwa kuwapiga na kitu kizito na baadaye kwenda kuitelekeza miili katika maeneo tofauti.

Jaji Mrisha alibainisha kuwa katika maelezo ya onyo yaliyotolewa, mshtakiwa alikuwa na mgogoro na baba yake mdogo, Danford Nziku ambaye ndiye baba ya watoto watatu waliouawa ambao ni Giliad Nziku, Gaspa Nziku na Godliver Nziku.

Pamoja na mshtakiwa kukana kuhusika na mauaji pamoja na kukana kuwafahamu watoto waliouawa, mahakama imesema kupitia vielelezo na mashahidi tisa walioapa na kutoa ushahidi mahakamani, mahakama imemkuta mshtakiwa na hatia ya mauaji kinyume cha sheria.

Alinukuu kifungu cha sheria namba 196 na 197 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16, marejeo ya mwaka 2022.

Jaji Mrisha alipomuhukumu Joel Nziku kunyongwa hadi kufa, aliagiza gari lililotumika kutekeleza mauaji litaifishwe na kuuzwa kupitia mnada na fedha zitakazopatikana ziwekwe kwenye akaunti ya serikali.

# Mpango kuendeleza ujuzi kwenye usalama wa mtandao wazinduliwa

**Na Halfani Chusi**

KATIKA kuisaidia nchi kufikia malengo kukuza uchumi wa kidijitali na kuchangiza Maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Benki ya Stanbic imezindua mpango maalum wa kuendeleza ujuzi kwenye usalama wa mtandao ili kuondoa upungufu uliopo katika eneo hilo.

Uzinduzi wa mpango huo unaoitwa ICT Skills Development Program (ISDP) ulifanyika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) hivi karibuni na kushuhudiwa na wanafunzi na wakufunzi wa chuo hicho.

Akizungumzia uzinduzi huo, Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wa Benki ya Stanbic, Mussa Ally alisema: "Sisi kama taasisi tunatambua umuhimu wa kuchangia katika maendeleo ya jamii zetu. Tunajivunia kuzindua mpango huu kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma." Alisema kupitia mpango huo, Benki ya Stanbic itafadhili mafunzo maalum ya kuongeza ujuzi kwa wanafunzi 10 bora na hivyo kuwafanya watambulike katika ulimwengu wa TEHAMA na utawafungulia milango ya fursa kwa kuwaandaa kuwa wajuzi watakaoshindana katika soko la ajira.

Makamu Mkuu wa UDOM, Prof. Lughano Kusiluka, aliwataka wanafunzi kujiunga na mpango huo ili kutimiza ndoto ya chuo hicho kuwa kitovu cha TEHAMA nchini.

Mkuu wa Kitengo cha Usalama wa Mtandao (Cyber Security) katika Benki ya Stanbic, Jumanne Makame alisema: "Kumekuwapo ongezeko la changamoto za tishio la kiusalama mtandaoni ambazo zinahitaji kuzalisha wataalamu watakaotuongezea ulinzi kwenye ulimwengu wa digitali.

"Ninawahimiza kuichukulia fursa hii kama hatua muhimu ya kuwaandaa kuwa viongozi katika ulimwengu wa mtandao. Ujuzi wenu ndio itakuwa ngao yetu kwenye mtandao na tunaamini mtafanya vitu vikubwa," alihimiza Alisema mpango huo unawapa wanafunzi vitu tofauti na mafunzo ya darasani. "Tuna nia ya dhati kuandaa askari watakaoongeza nguvu katika ulinzi wa kidigitali. Tumechagua Chuo Kikuu cha Dodoma kwa sababu tunaamini uwezo wenu wa si tu kuzalisha wahitimu bali viongozi mahiri kwenye masuala ya usalama wa mtandao," alisema



Daktari wa Idara ya mifupa, Kitengo cha miguu kifundo katika Hospitali ya CCBRT, Dk. Anigod Munisi (mwenye shati ya bluu) na Muuguzi wa idara hiyo, Robinson Mapunda wakimhimiza mtoto Arafat Hussein (5), kutembea mbele ya wageni baada ya kumalizika kwa matibabu yake ya miaka mitano ya miguu kifundo kwa mafanikio makubwa, wakati CCBRT ilipowakutanisha wadau wake hospitalini hapo, Dar es Salaam jana, kwa lengo la kuwashukuru kwa kuunga mkono jitihada za kuwahudumia watanzania wenye changamoto za kiafya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



## Kata Madimba, Msimbati mbioni kupatiwa umeme

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAKALA wa Nishati Vijijini (REA) umeanza utekelezaji maagizo ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko ya kuwafikishia huduma ya umeme wakazi wa Madimba na Msimbati.

Katika kutekeleza maagizo hayo jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Nishati Vijijini, Balozi Meja Jenerali mstaafu, Jacob Kingu alifanya ziara ya kufanya tathmini katika kata za Madimba na Msimbati ili kuona hali halisi kabla ya kuanza utekelezaji.

Akizungumza na madiwani wa kata hizo, Balozi Kingu alisema REA itahakikisha maelekezo hayo yanatekelezwa. Imeanza kwa kukutana na mkandarasi kujadili ujenzi wa miundombinu ya umeme katika kata hizo.

"Tutahakikisha utekelezaji wa haraka unafanyika na wataalamu wanapita ili kuona hali halisi na uhitaji katika maeneo husika," alisema.

Aliwataka wananchi wa maeneo hayo kuwapatia ushirikiano wataalamu wa REA na mkandarasi huyo ili kuharakisha uratibu wa kazi hiyo.

Aliagiza taarifa zitolewe haraka endapo kutakuwa na changamoto katika utekelezaji wa mradi huo zipatiwe ufumbuzi.

Mkurugenzi wa Nishati Vijijini, Jones Olotu aliwahakikishia maofisa watendaji wa kata hizo wiki ijayo makandarasi watafika kukutana nao kwa ajili ya kuoneshwa maeneo na vijiji vinavyotakiwa kupata umeme.

Diwani wa Msimbati, Rashid Linkon na Diwani wa Madimba, Idrisa Kujebweja, waliishukuru serikali kwa uamuzi wake wa kuhakikisha wanapata umeme na kunufaika na rasilimali ya gesi asilia inayopatikana eneo hilo.

Akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Mtwara hivi karibuni, Dk. Biteko aliitaka REA kuangalia namna ya kuwaunganishia umeme wananchi wa maeneo hayo na kujenga miundombinu ili wanufaike na gesi asilia katika eneo hilo.

# CCM yang'aka miradi ya maji kukwama, yamtega Aweso

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma imekerwa na kukwama utekelezaji miradi ya maji wilayani Bahi kikitaka wahusika wawajibishwe.

Katibu wa Siasa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo mkoani humo, Jawadu Mohamed alitoa kauli ya kutaka kuwajibishwa kwa wahusika wakati wa ziara ya kamati hiyo ya kukagua utekelezaji miradi ya maendeleo.

Alikuwa anazungumza na baadhi ya viongozi wa CCM na serikali baada ya kukagua miradi hiyo wilayani Bahi, ukiwamo wa maji wa Kata ya Chali unaotarajia kugharimu Sh. bilioni 2.3 mpaka kukamilika.

Katibu huyo alisema CCM hakiwezi kuvumilia kuona wananchi wanaendelea kuteseka kwa kukosa maji wakati kiliahidi kusogeza huduma muhimu kwenye makazi yao, hivyo wanaokwamisha wanapaswa kuwajibishwa. Alisema tatizo la maji limekuwa kubwa mkoani Dodoma kutokana na maelekezo ya serikali kupuuzwa.

"Hatuwezi kuwa na makao makuu ambayo watu hawaogi, hawafui na wanatumia muda mwingi kutafuta maji. Tunakwenda kuandaa mkakati wa taarifa rasmi juu ya upatikanaji maji kwenye kata zetu zote 209 za Mkoa wa Dodoma.

"Kama Mheshimiwa (Jumaa) Aweso (Waziri wa Maji) mambo ya maji yamemshinda, basi ninaamini zipo wizara zingine ambazo ataweza, lakini ninaamini bado anaweza na kama kuna tatizo kwa watendaji wake awabane," alisema Mohamed.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM Mkoa wa Dodoma ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa Mkoa huo, Samwel Malecela, alisema chama hicho hakiwezi kuvumilia kuona maelekezo ya viongozi wake wa juu yanapuuzwa huku akiwaomba radhi wakazi wa Kijiji cha Chali kwa kuendelea kukosa huduma ya maji.

"Ipo sababu ya kuwaombeni radhi sana kutokana na maumivu na sisi tunasikia na kama tukiona miradi ya maji haitekelezeki hatuwezi kuliacha hivihivi, viongozi wanatoa maagizo," alisema.

Awali akitoa taarifa ya mradi wa maji wa Kata ya Chali mbele ya kamati hiyo, Meneja wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Robart Mgombelwa, alisema ukikamilika utatoa huduma kwa vijiji vitatu vyenye watu 13,000. Mgombelwa alisema mradi huo ulianza kutekelezwa Juni mwaka jana na kutakiwa kukamilika Julai mwaka huu, lakini umekwama kutokana na kukosa fedha.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza katika mkutano wa pili wa Jukwaa la Sauti ya Nchi Zinazoendelea, uliofanyika kwa njia ya mtandao, jijini Dodoma, jana. Majaliwa amemwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika Mkutano huo ambao umefunguliwa na Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi. **PICHA: OWM**

# Mpango wa chakula shule za msingi wazinduliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imezindua mpango wa utekelezaji wa mwongozo wa kitaifa wa utoaji huduma ya chakula na lishe kwa wanafunzi wa shule za msingi kwa lengo la kudhibiti utoro na kuongeza kiwango cha ufaulu nchini.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe wakati wa hafla ya uzinduzi wa mpango huo jijini hapa jana, alisema utekelezaji mwongozo huo unategemea ushiriki wa makundi yote ikiwamo wazazi, serikali na wadau wengine wa maendeleo.

"Wazazi wanapopanga bajeti zao za chakula nyumbani hawana budi kutambua kuwa ipo haja wao pia kutenga bajeti kwa ajili ya watoto wao kupata chakula wanapokuwa shuleni ili kuwawezesha kushiriki vipindi na kuondokana na tatizo la utoro," alisema Prof. Mdoe.

Alisema utoaji wa chakula shuleni ni jambo muhimu katika kuwasaidia watoto kushiriki masomo kwa mujibu wa ratiba ili kuongeza kiwango cha ufaulu.

"Chakula ni kitu muhimu sana kwa kila mtu, hivyo kuwapo mwongozo huu wa utoaji wa chakula na lishe shuleni kutakuwa msaada mkubwa kwa watoto wetu katika ushiriki wao wa masomo na kuwaongezea usikuvu tofauti na ilivyo sasa," alisema.

Mtendaji huyo wa wizara alisema wizara hiyo itaendelea kushirikiana kuhamasisha wazazi na wadau wengine kuchangia kwenye shule zote nchini ili watoto wote wapate chakula kwa asilimia 100.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Rogatus Mativila, alisema serikali inatambua mchango wa wataalamu kutoka wizara, taasisi na wadau walioshiriki kuandaa mpango huo.

"Kwa kipekee Ofisi ya Rais - TAMISEMI inatoa shukrani za dhati kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) kwa kufanya sensa ya utoaji huduma ya chakula na lishe katika shule za msingi nchini, " alisema Mativila.

Alisema matokeo yaliyopatikana na kuwasailishwa serikalini ni chachu katika utekelezaji utoaji huduma ya chakula na lishe shuleni.

"Serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa kuchapisha nakala 33,000 za vitabu ambavyo vinazinduliwa leo (jana) kwa ajili ya kusambazwa katika shule zote za msingi na sekondari nchini," alisema.

Mativila alisema vitabu hivyo vitawezesha kuweka malengo ya mwongozo wa utoaji huduma ya chakula na lishe katika vitendo kwa ajili ya utekelezaji.

Pia alisema kwa sasa utoaji wa chakula na lishe shuleni umegawanyika katika makundi mawili.

Alisema kundi la kwanza ni la wanafunzi wa bweni ambao wanahudumiwa na serikali na lingine ni wanafunzi wa kutwa ambao wanahudumiwa na wadau wakiwamo wazazi, jamii, taasisi za dini na kampuni.

Hata hivyo, alisema ufanisi wa kazi hiyo unatokana na fedha zinazotengwa na serikali kila mwaka.

"Mfano mwaka 2020/21 Sh. bilioni 124.3 zilitumika, mwaka 2022/23 Sh. bilioni 141.8 zilitumika na mwaka 2023/24 Sh. bilioni 145.4 zinaendelea kutumika," alisema.





# Wawekezaji wapewa jukumu kurejesha Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii ameelekeza wawekezaji katika sekta ya utalii kujikita kwenye utunzaji mazingira ili kurejesha hadhi ya Zanzibar ya kijani.

Hafsa Mbamba alitoa rai hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari baada ya ufunguzi wa warsha ya wawekezaji na wadau wa mazingira kuhusu uhifadhi wa mazingira ikiwa ni mwendelezo wa tamasha la Zanzibar ya Kijani lenye lengo la kuendeleza na kusisitiza utalii endelevu.

Hafsa alisema kuna umuhimu kwa wawekezaji kuleta utalii endelevu wenye Zanzibar ya Kijani ili chakula kinachopatikana visiwani hapa kiwe endelevu, ikiwamo mboga, viumbe vya baharini na samaki vinavyotumika katika hoteli za kitalii badala ya kuagizwa nje ya visiwa ya Unguja na Pemba.

Alisema umefika wakati wa kudhibiti taka na matumizi ya plastiki, kulinda urithi, kuzingatia matumizi ya silka na tamaduni katika sekta ya utalii, kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, kutumia miti ya asili katika bustani kwenye hoteli na utunzaji mazingira.

Hafsa alisema warsha hiyo imewashirikisha wamiliki wa hoteli hizo kwa sababu sekta ya utalii duniani ndiyo inayozalisha taka nyingi ikiwamo plastiki, hivyo ni vyema kuelimisha jamii kuwa ni fursa na njia mbadala ya kupata ajira.

Miza Suleiman Khamis, Ofisa Mkuu Idara ya Misitu Zanzibar, aliwataka wawekezaji katika sekta ya utalii kutohamisha uoto wa asili wakati wanapofanya uwekezaji ili kulinda mazingira.

Khamis alisema uhalisia wa Zanzibar una uoto wa asili, hivyo kama ukiondolewa viumbe hai wa bayoanuai watakosekana kwani wanasaidia utunzaji wa mazingira.

Alisema si watalii wote wanaofika Zanzibar wanapenda fukwe, wengine wanavutiwa na mazingira mazuri yenye miti na uoto wa asili, hivyo ni vyema wawekezaji wanapojenga hoteli zao kuacha uhalisia wa uoto huo.

Alisema Hoteli ya Sharzad ni mfano wa kuigwa katika utunzaji wa mazingira kwa sababu viumbe hai vinapatikana katika hoteli hiyo, ikiwa ni pamoja na kima punju kutokana na kulinda na kuhifadhi miti na uoto wa asili.

"Wawekezaji wengi wa hoteli wanaojenga hukata miti yote iliyokuwepo awali hali inayopoteza uhalisia wa Zanzibar ya Kijani," alisema Khamis.

Alisema baadhi ya watalii wanafika visiwani hapa kujifunza mila na tamaduni, hivyo ni vyema wawekezaji wa sekta ya utalii kulinda mila, silka na tamaduni za Mzanzibari ili kuwavutia watalii wengi.

Alisema katika kulinda na kuhifadhi mazingira ili kurejesha Zanzibar ya Kijani lazima kuwa na ushirikiano katika sekta ya ardhi, utalii, uwekezaji na mazingira na kusimamia miongozo ambayo itasiadia kulinda uoto wa asili.

Mtaalamu wa Miti wa Idara ya Misitu, Rose Hillary, alisema miti ni muhimu kwani inasaidia kuzuia mmonyoko wa ardhi na kudhibiti kasi ya mawimbi kwenye fukwe.

Mwekezaji wa Hoteli ya Sharazad iliyoko Jambiani, Francesia Scalfor, alisema ni rafiki wa mazingira na wanapambana kudhibiti matumizi ya plastiki na kupanda miti ya asili katika maeneo yanayowazunguka.

Alisema ardhi inalindwa na taka za majani, hivyo watu wengi wanafanya makosa ya kuondoa majani kwani yanasaidia viumbe hai kuendelea kuishi na ardhi kuwa rutuba.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ, Masoud Ali Mohamed (katikati), akizungumza na wageni kutoka Manispaa ya Jiji la Chongqing, nchini China, ofisini kwake Vuga Zanzibar jana, wakiwa katika ziara maalum ya kuimarisha undugu na kubadilishana uzoefu. **PICHA: MAELEZO-ZNZ**

## SMZ, China kuimarisha ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imesema itaimarisha zaidi ushirikiano wake na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ili kukuza uchumi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Mohamed alipozungumza na Naibu Meya wa Manispaa ya Jiji la Chong Qing, China, ofisini kwake Vuga.

Mohamed alisema SMZ na China ni marafiki wa muda mrefu, hivyo wataendelea kushirikiana kwa lengo la kuleta maendeleo nchini.

Alisema ugeni huo una lengo la kuzisaidia manispaa visiwani hapa na kubadilishana uzoefu wa utendaji kazi ili kuhakikisha Jiji la Zanzibar linakuwa na mazingira mazuri.

"Kama tunavyoelewa kuwa wenzetu wa Jamhuri ya Watu wa China wamepiga hatua kubwa sana katika kuipendezesha miji yao, lazima tujifunze kutoka kwao," alisema.

Naibu Meya wa Chong Qing, Shang Kiu aliahidi kuwa ushirikiano huo utakuwa endelevu ili kuleta manufaaa kati ya nchi hizo.

Mstahiki Meya wa Jiji la Zanzibar, Mahmoud Mohamed Mussa, alisema ujumbe huo una nia thabiti ya kushirikiana na kusaidiana kuupendezesha Mji wa Zanzibar.

Mussa alisema katika kupendezesha Zanzibar na kuwa mji safi, kuna hitajika kuboresha na kuimarisha miundombinu iliyopo.

Ujumbe huo ambao ulikuwa katika ziara ya siku mbili ulitembelea maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja ma kuangalia mazingira ya mji na vivutio vya utalii vilivyopo.

# Mtakwimu Mkuu ataka wadau kuimarisha uchumi wa Afrika

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MTAKWIMU Mkuu wa Serikali ya Zanzibar, Salum Kassim Ali amewataka wadau wa takwimu za biashara na uchumi kujiimarisha katika mifumo ya ushirikiano wa kiuchumi barani Afrika ili kukuza biashara visiwani hapa na kuleta tija.

Alitoa rai hiyo jana wakati wa kikao na wadau wa takwimu za biashara na uchumi, alipozungumzia Wiki ya Siku ya Takwimu Afrika.

Ali alisema wakati huu mataifa yamo katika kuadhimisha takwimu za Afrika, hivyo ni lazima nchi hizo kuwa kitu kimoja katika uzalishaji na uuzaji wa bidhaa zao kwa bara hilo.

Mtakwimu huyo, alisema wakati mataifa ya Afrika yakijadiliana juu ya ufanyaji biashara kwa mataifa husika, ni vyema Zanzibar ikajipanga kuhakikisha inazalisha biashara bora na kuingia katika soko la ushindani duniani.

Alisema kuna changamoto kubwa kwa upande wa takwimu hasa wanaotumia mitandao kukosa uhalisia wa takwimu sahihi na kutoa takwimu ambazo si sahihi.

Wadau wa takwimu za uchumi na biashara Zanzibar walisema eneo huru la biashara la Afrika ni kuwa na soko la pamoja kutokana na bara hilo bado kuwa nyuma kwa ununuzi, hivyo ni vyema kutengeneza biashara zao ili kupunguza ushuru wakati wa kusafirisha.

Walisema katika kuhakikisha biashara za Afrika zinakuwa ni lazima kuzalisha biadhaa zenye ubora ili kuendana na wakati wa sasa wa teknolojia.

Haji Abdullah, miongoni mwa wadau hao, alisema Zanzibar inaingiza kiwango kikubwa cha bidhaa kutoka nje tofauti na wanachokitoa kupeleka katika mataifa mengine na kusababisha uchumi wa Afrika kuwa na changamoto.

Alisema Afrika ni bara la pili kwa ukubwa duniani, lakini imekuwa changamoto kupeleka bidhaa zao katika mabara mengine hasa kutokana na kukosa ubora.

Alisema moja ya kampeni kwa mabara ya Ulaya ni kuondoa viza kwa raia kwenda kutembea na kufanya biashara ndani ya maeneo hayo tofauti na Afrika ambako viza zinatumika.

"Zanzibar inategemea kuzalisha uchumi wake kupitia utalii na karafuu, lakini mpaka sasa kuna nchi ngapi zinaingiza karafu kama za Zanzibar, lazima watu wa takwimu kuwa na utayari kujua takwimu hizo," alisema.

Aliongeza kuwa ili kufikia hatua ya kukuza biashara kwa upande wa Afrika, nchi zinatakiwa kuwa kitu kimoja katika kupanga mipango yake ya kiuchumi na kushirikiana.

Kaulimbiu ya wiki ya Siku ya Takwimu Afrika kwa mwaka huu ni 'Uboreshaji mifumo ya ushirika wa kitakwimu ili kurahisisha utekelezaji wa eneo huru la biashara la Afrika'.



# HAWANA BAYA Wanune lakini ndio hivyo....

MASHABIKI wengi wa muziki nchini wanatarajia kuona matokeo mazuri kufuatia mastaa wawili ambao huko nyuma walikuwa katika lebo moja ya WCB kuamua kuondoa tofauti zao.

Hivi karibuni Rayvanny alitangaza yeye na Harmonize wamekaa kwa pamoja na kuamua kuanza ukurasa mpya wa maisha na kuachana na tofauti zao za zamani.

Katika maelezo yake, Rayvanny amekiri kwamba huko nyuma walikuwa na tofauti nyingi ikiwa zingine kutokana na utofauti ya mitazamo na zingine kwa kufanya makusudi.

"Tuliongea kama watu wazima tukakubaliana hatutakiwi kugombana, yeye sawa na kaka muda wa kugombana umekwisha kilichobaki tufanye kazi," amesema Rayvanny.

Kutokana na kauli hiyo baadhi ya wadau wa muziki wa kizazi kipya, wamesema tangazo hilo limewapa faraja na wana matumaini wawili hao watatoka na kazi ya pamoja.

Baraka Jerrson amesema kitendo cha Rayvanny kuelezea mpaka tuzo alizopata Harmonize na kumuunga mkono ni ishara kwamba wawili hao hawana ugomvi tena.

"Huko nyuma haikuwa rahisi kwa wasanii hawa kuelezana mambo mazuri, lakini kwa sasa ni tofauti natarajia watatupa kitu kizuri kama zawadi," amesema.

Mwijaku kwa upande wake amesema ni jambo zuri kumuona Rayvanny akimkubali Haronize hadharani na kwamba anamkaribisha na kuwa mapacha wawili wanaofanana.

"Amechelewa kuondoa tofauti zao, lakini kama mdogo wangu nampongeza kusema hadharani kwamba wameyamaliza, namshauri wafanye kazi kama mapacha na kuleta ushindani katika muziki," amesema Mwijaku.

## BASI SAWA

### Profesa Charugamba kukamilisha albamu 16



MWIMBAJI mkongwe wa Injili nchini, Profesa Ussy Charugamba, amesema yuko mwishoni kukamilisha albamu yake ya 16 baada ile ya 15 kufanya vizuri.

Akizungumza na BT, Charugamba alitamba kuwa yeye anaongoza kuwa na albamu nyingi kuliko mwimbaji yoyote wa injili na zimebadilisha maisha ya watu.

"Hiki ni kipawa ambacho ninakitumia vizuri, mimi ndio mwimbaji wa injili mwenye albamu nyingi, sasa nina albamu 15 najiandaa kufanya albamu ya 16 ambayo itakuwa ya moto kuliko zingine," alisema Charugamba ambaye ni wakili msomi.

### Jitu Baya ahimiza kuvuka 'Border'



MKALI wa Hip hop, Jitu Baya ametambulisha ngoma yake mpya inayokwenda kwa jina la Border maalum kwa watu wanaopambana na maisha.

Jitu Baya amesema wimbo huo umerekodiwa chini ya prodyuza Fresh Boy umeanza kusikika na mashabiki kupitia vituo vya redio na majukwaa ya muziki mtandaoni siku tatu zilizopita.

"Border ni wimbo wa kuwapa hari watu wanaopambana kutafura mafanikio kama ilivyokuwa kwa Rais wetu Samia Suluhu hassan anavyofanya kutuhangaikia ili Watanzania tufike mbali," amesema Jitu Baya.




## WHOZU AAPA KUTORUDIA KOSA

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Whozu amesema hatorudia kuandaa video inayoweza kumuingiza matatani na kuharibu mipango yake ya kazi.

Amesema kifungo chake cha miezi sita asijihusishe ambacho serikali ilitengua na kumpiga faini, kilimnyima usingizi kutokana na kuwa na makubaliano kufanya kazi nne mwezi ujao hadi Januari mwakani.

"Sikupata usingizi baada ya kufungiwa, nilikuwa na kazi nne nimeshakubaliana nao nilijiuliza nitafanyaje, lakini naishukuru Basata kunionea huruma na kutufungulia. Sitarudia tena nitakuwa makini," amesema Whozu.



## Unaujua 'Karola' wa Remy Ongala?

MSANII wa muziki wa dansi Karola Kinasha, amesema tamasha la Ongala lina umuhimu katika maisha yake kutokana na ukaribu wake na mwanamuziki mkongwe marehemu Dk.Remi Ongala.

Amesema Remi alitunga wimbo maarufu unaoitwa Karola kutokana na jina lake kama ishara ya kumkubali na kumthamini.

"Wimbo ule aliutunga wakati akijiandaa kwenda kwenye ziara ya muziki nchini Uingereza, ni muhimu kumkumbuka kwa kutumia tamasha hili," amesema.

Mwaandaaji wa tamasha hilo, Aziza Ongala amesema 'Ongala Festival' litakalofanyika Novemba 24 hadi 26 jijini Dar es Salaam na lengo lake ni kuendeleza ndoto za baba yao katika kazi za musiki.

## FILAMU

# Nyaso: Jicho la Mchawi

**Na Adam Fungamwango**

FILAMU inaitwa 'Nyaso.' Inaakisi baadhi ya visa na mikasa iliyo kwenye jamii na familia zetu kwa ujumla.

Kijana wa kiume anaweza kumpenda binti fulani, lakini kwa sababu wanazozijua wenyewe, wazazi hawataki.

Binti anaweza kutaka kuolewa na kijana fulani, lakini wazazi wanapinga, utafikiri wao ndiyo wanakwenda kuishi nao.

Imechezwa na wasanii, Zubeda Mkokola, Hamis Korongo, Fatuma Makongoro na wengineo.

Kijana mashaka, anatokea kumpenda binti mmoja aitwaye Nyaso. Ni binti nzuri na mrembo ambaye vijana na watu wazima wanammezea mate kijijini hapo.

Binti mwenyewe amekufa na kuoza kwa Mashaka. Mzee Korongo naye anajitosa kwenda nyumbani kwa Bi. Fatuma kumposa Nyaso. Mama yake akakubali kwa sababu hajawahi kupata barua kutoka kwa mtu yoyote anayemhitaji binti yake zaidi ya mzee Korongo.

Binti naye hamtaki mzee, anamtaka kijana mwenzake, anakimbia haraka kumwambia Mshaka kuwa ahawahishe barua kabla ya mzee Korongo haijafika.

Kijana anafanya hivyo, lakini anapifika anatolewa 'balu' na mama Nyaso. Mama anamtaka mzee Korongo kwa sababu ana mashamba na pesa.

Na alivyosema yeye ni mtoto wa mzee Kibaya ndiyo kabisa akamvuruga. Binti anapigwa mkwara kuwa lazima aolewe na mzee Korongo. Bado binti akagoma.

Kwa mzee Kibaya naye, Mashaka akamwambia baba yake kuwa anataka kumchumbia Nyaso, binti na Bi. Fatuma. Baba akawaka na kusema aachane naye na hatokuwa na radhi naye.

Mashaka na Nyaso wakaanza kufitinishwa kwa njia ya kishirikina. Wakikutana, kijana nguvu za kiume zinapotea na binti tumbo linaanza kumuuma.

Hatimaye inakuja kugundulika kuwa miaka mingi nyuma, kumbe mzee Kibaya na Bi. Fatuma waliwahi kugombea shamba, kwa maana hiyo Kibaya akamwambia aachane kabisa na Nyaso.

Kijana anafanya hivyo, anaandika barua kwenda kwa Nyaso kuwa hamtaki tena. Barua hiyo inamchanganya binti na kulazimika kumkubali mzee Korongo.

Siku ya harusi binti haonekani, ametoroka. Wakati wanashangaa binti anajitokeza na kuwaambia waliohudhuria kuwa mambo yote yaliyojitokeza yalitengenezwa na mama yake, mzee Korongo na mzee Kibaya, kila mmoja akiwa na lake ili kuwafitinisha. Akamkumbatia mpenzi wake Mashaka akisema ndiye atakayeolewa naye.




## ALIYEACHWA SOLEMBA ANAVYOTRENDI

**Na Adam Fungamwango**

MUZIKI una kazi kubwa sana duniani, ya kuelemisha, kuburudisha, kuonya na hata kufikisha ujumbe kwa njia mbalimbali. Ujumbe wa muziki hufika vizuri na hukaa kwenye vichwa vya watu zaidi kuliko ukitolewa kwa njia nyingine kama hotuba, risala au kitu kingine.

Mwanamuziki au msanii anaweza kuchomekea au kuongea neno ambalo likazua msamiati ambao ukatumika kwenye jamii kwa muda mrefu au moja kwa moja vizazi na vizazi.

Mfano ni msanii Mwana FA, ambaye kwa sasa ni Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma, yeye alifyatua ngoma nyingi ambazo majina yake yalizua misamiati mitaani kwa kizazi hiki.

Ngoma hizo ni kama 'Bado Nipo Nipo', 'Habari Ndiyo Hiyo', 'Asanteni Kwa Kuja', 'Unanitega', na nyingine nyingi.

Katika muziki wa dansi tangu miaka ya 1970 hadi 1990 kuna nyimbo ambazo zilitengeneza misamiati mitaani iliyotumika kama neno halisi.

**Solemba-Juwata Jazz Band**

Msemo ambao umeshakuwa kama msamiati, solemba unatumiwa na hata watoto wa vizazi vya sasa kuonyesha, yeyote aliyekwenda kwa mpenzi wake au kupeana ahadi alipofika akaambulia patupu. Hakumuona au hakutimiza ahadi.

Wimbo huu ulitungwa na marehemu Nico Zengekala akiwa na bendi ya Juwata Jazz.

Unaelezea jinsi jamaa alivyoitwa na msichana aitwaye Solemba aende kwao, lakini alipofika huko alimkana. Ndiyo maana yeyote anayedanganywa na mpenzi wake au kuambiwa wakutane sehemu fulani, halafu mwingine hakwenda, basi ataambiwa tu "Ameachwa solemba."

**Libeneke-Butiama Jazz Band**

"Unajua wewe unaendeleza sana libeneke." Ni msamiati fulani ambao upo hadi leo. Nadhani wengine wanautumia bila kujua maana yake. Mtu yeyote anayeonekana kufanya kitu bila kiasi, kila kitu anakifanya kupitiliza anaambiwa anaendeleza libeneke.

Ulitokana na wimbo wa Butiama Jazz Band unaoitwa 'Mtindo Libeneke'. Libeneke ni mtindo wa bendi hiyo kama ilivyo Msondo Ngoma au Sikinde ngoma ya ukae. Libeneke ni ngoma moja ya kienyeji Ifakara.

Wanatajana majina wanamuziki wote wa bendi hiyo, na kuna kipande wanaimba "Waache waseme watachoka wao sisi tupo tunaendeleza libeneke." Wakiwa na maana wanaendeleza bendi yao yenye mtindo huo. Ndipo ulipozaliwa msemo huo.

**Huna-Marijani Rajab**

Neno 'Huna' lilizaa msamiati maarufu sana katikati ya miaka ya 1970 hadi mwanzoni mwa 1980. Mwanamke kama hamtaki mwanaume anayemuomba urafiki kwa namna yoyote ile, iwe hamtaki tu, au hata pesa, basi atamjibu 'huna'. Neno hilo peke yake lilitosha kumpa ujumbe mwanaume kuwa hatakiwi. Lilitokana na wimbo 'Hanifa' ambapo mbele kuna kimsemo hicho kilichotrendi kweli kweli miaka hiyo.

"Eee bwana huna (huna), hakutaki tena ee, baba na mama, na mume mwanangu huna." Kiliimbwa hivyo.

**Moja moto, Moja baridi- Mlimani Park**

Msamiati huu ulitumiwa sana miaka ya 1980 na watu wa kawaida na hata wanaokwenda baa kunywa.

Wakifika watasema, "lete moja moto moja baridi." Mwingine atamwambia mwenzake, nilienda kupata, "moja moto moja baridi', yaani alikwenda kunywa.

Ulitokana na wimbo uitwao 'Kassim' wa Orchesta Mlimani Park.

Kuna baadhi ya maneno yanayoimbwa, "unapotoka kazini unapitia kwenye baa, unapokuta marafiki, ukiagiza moja moto moja baridi."



# Jennifer amlilia Matty

MWIGIZAJI kutoka Marekani Jennifer Aniston amesema sura ya mpenzi wake Matthew Perry, ambaye alifariki Oktoba 28, bado inamsumbua anapokuwa amelala.

Akiandika kupitia ukurasa wake wa Instagram, msanii huyo alichapisha picha yake akiwa na mpenzi wake huyo wakitabasamu wakati wakicheza filamu ya Friends, na kuelezea akikumbuka nyakati ambazo yeye na wenzao walikuwa wakicheka walipoigiza kama wahusika wakuu.

" Kumuaga Matty kumekuwa na wimbi la hisia za wendawazimu ambalo sijawahi kupata hapo awali. Kupoteza maisha au kupoteza upendo unabaki kukaa na huzini milele," ameandika Jennifer.



## Oladips hatunaye tena

RAPA kutoka Nigeria Oladips amefariki dunia baada ya kuugua kwa miaka miwili.

Uongozi wa mwanamuziki huyo mwenye umri wa miaka 28, ulitoa tangazo la kifo chake na kueleza katika kipindi hicho Oladips alikuwa akipatiwa matibabu ya siri ya ugonjwa uliokuwa ukimsumbua kwa muda mrefu.

"Tunasikitika kuwafahamisha umma kuwa Oladipupo Olabode Oladimeji maarufu kama Oladips alifariki. Bado tuna mshtuko tunapozungumza kuhusu msiba huu," imesema taarifa hiyo.

## Wanaomtetea Smith waonyesha hasira

TIMU ya mwigizaji Will Smith imesisitiza kumburuza mahakamani Brother Bilaal, kutokana na kumzushia uongo kwamba msanii huyo maarufu anajihusisha na mapenzi ya jinsia moja.

Bilaal alidai kwamba alimfumania Smith akishiriki ngono na rafiki yake Duane Martin.

Watu wanaomsimamia Smith waliambia mtandao wa TMZ kwamba madai hayo hayana ukweli na yametungwa kwa nia ya kumchafua msanii huyo.

"Hadithi hii imetungwa kabisa ni ya uwongo usio na shaka, tutamchukulia hatua za kisheria Bilaal kutokana na kashfa hii." ilisema timu hiyo.





## Rihanna kazidi kuwashangaza

MASHABIKI na wapenzi wa mwanamuziki maarufu wa Marekani, Rihanna wameshangazwa kutokana na maamuzi yake ya kubeba ujauzito haraka.

Rihanna na mume wake ASAP Rocky wanatarajia kupata mtoto wa tatu, ikiwa ni miezi mitatu pekee tangu ajifungue mtoto wa pili.

Katika mitandao ya kijamii watu wamegawanyika katika maoni yao ikiwa wengi wanaonyesha mshangao kwa nini msanii huyo kabeba ujauzito haraka bila kujali ustawi wa kichanga chake.

## Harrysong amejitakia balaa

IMEELEZWA mwanamuziki wa Afrobeat wa Nigeria, Harrysong itambidi kulala na mwanamke tofauti kila siku ndani ya mwezi mmoja ili kutimiza masharti ya ndoa.

Harrysong hivi karibuni amevunja rekodi baada ya kufunga ndoa na wanawake 30 kwa siku moja.

Awali rekodi hiyo ilishikiliwa na nguli wa muziki huo, Fela Anikulapo Kuti kwa kuoa wake 27 kwa wakati mmoja.

Kulingana na wachambuzi katika masuala ya ndoa nchini humo, walieleza mwanamuziki huyo hatoweza kurudia kulala na mwanamke mmoja ndani ya mwezi mmoja ili kuweka mzunguko mzuri wa ndoa za wake wengi na kuepuka malalamiko.







# Prof. Mkumbo: Anayekwaza uwekezaji ni adui wa uchumi

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji amewataka Watanzania kujenga imani kwa Rais Samia Suluhu Hassan kuhusiana na kauli yake ya kutaka kuifungua nchi.

Prof. Kitila Mkumbo amesema lengo la Rais Samia ni kuondoa uadui wa kibiashara na kuweka mazingira mazuri na bora ya biashara na uwekezaji nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Prof. Mkumbo alisema jana kuwa lengo la serikali ni kutaka kuona biashara na uwekezaji havipati vikwazo katika utekelezaji wake.

"Kazi za msingi za serikali ni kutengeza mazingira mazuri katika biashara, biashara ndiyo huzaa ajira na ajira huzaa fedha, hivyo lazima serikali ihakikishe biashara inafanyika.

"Mheshimiwa Rais aliposema anakwenda kufungua nchi, alimaanisha anaweka mazingira bora ya biashara na uwekezaji," alisema.

Alisema kuwa katika upatikanaji ajira nchini, kati ya 100 zinazotengenezwa ni tano tu zinatokana na Serikali na nyingine 95 zinatengenezwa na sekta binafsi.

"Kwahiyo, mtu yeyote ambaye anakwaza sekta binafsi kuwekeza mahali anapotaka, huyo ni adui wa maendeleo ya uchumi na ajira, mara nyingi tumekuwa tunajiuliza kwanini nchi ambazo zimeendelea bado zinapiga hatua na ambazo hazijaendelea zinabaki kuwa maskini.

"Sababu ya msingi kuliko zote ni kwamba nchi zilizoendelea zimejikita zaidi kibiashara na uwekezaji, maadui watatu tangu uhuru ni maradhi, ujinga na umaskini, ni lazima tupambane na tuwashinde hawa maadui," alisema.

Vilevile, alitoa maelezo manane kwa Mkoa wa Tanga, wilaya na halmashauri zake kuhusu utendaji kazi kuanzia mamlaka za serikali za mitaa.

"Mamlaka zote zinazohusika na uwekezaji ziondoe urasimu usio wa lazima kiasi cha kuwakatisha tamaa wawekezaji. Mkuu wa Mkoa simamia jambo hili.

"Pia Mamlaka zote za Serikali za Mitaa (halmashauri) zitenge maeneo mahususi ya kuyahodhi kwa ajili ya uwekezaji na kuyawekea huduma zote muhimu ikiwamo barabara, wakuu wa wilaya simamieni hili," aliagiza.

Prof. Mkumbo alisema mkoa unatakiwa uandae mkakati wa mawasiliano ili kuongeza kasi ya mawasiliano na kutangaza fursa za miradi zilizopo kwenye maeneo na kuwafikia wawekezaji wengi zaidi.

"Mipango yote ya uwekezaji izingatie maelekezo ya serikali ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira," alisema.

Kwa upande wa fursa za uchumi wa bluu, waziri huyo aliutaka mkoa kusimamia kilimo endelevu cha mazao ya bahari kutokana na kuwa ni kila aina ya samaki ili kuongeza mazao ya bahari na kumnufaisha kila mmoja.

Aliwahakikishia wawekezaji waliopo na wanaotarajiwa kuja kuwekeza Tanga, usalama wa kutosha na ushirikiano baina yao na serikali.

"Wawekezaji mliopo na wale mnaotaka kuja mnakaribishwa sana. Tanga ni salama na ushirikiano upo wa kutosha. Vilevile kwenu wakuu wa mikoa fuatilieni kwa karibu utekelezaji miongozo ya fursa ya uwekezaji.

"Lakini mwisho, wakurugenzi wa halmashauri zote nchini wekeni mikakati ya utekelezaji wa fursa zilizopo katika maeneo yenu kwa kwa kutumia miongozo ya mikoa na kubainisha fursa mpya za uwekezaji," aliagiza.

# Marufuku mabasi yasiyosajiliwa, bodaboda kubeba wanafunzi

**Na Steven William,** MUHEZA

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wilayani Muheza, mkoani Tanga limepiga marufuku wanafunzi wa darasa la awali na msingi kusafirishwa kwa mabasi yasiyosajiliwa kutoka nyumbani hadi shuleni kwa kuwa hayatambuliki kisheria.

Amri hiyo ilitolewa juzi na Kamanda wa kikosi hicho wilayani hapa, Leonard Bandora alipotoa elimu kwa wazazi na walimu ya ukaguzi na usalama wa mabasi ya kubeba wanafunzi katika kikao kilichofanyika Shule ya Msingi ya Holy Family inayomilikiwa na watawa.

Bandora alisema ni lazima wanafunzi watumie usafiri wa mabasi ya shule na ya watu binafsi ambayo yamesajiliwa kisheria na serikali yenye rangi ya njano.

Alisema uongozi wa shule unatakiwa kuhakikisha basi la kubeba wanafunzi asubuhi na jioni au wakodishe kwa watu binafsi ambao vyombo vyao vya usafiri vimesajiliwa ili watoto wao wawe salama dhidi ya vitendo viovu.

Alitoa wito kwa wazazi kutii sheria bila shuruti na kuacha kutumia bodaboda kama usafiri wa kubeba watoto huku wakiwa hawajavaa kofia za kinga.

Alifafanua kuwa kisheria mtoto wa chini ya umri wa miaka mitatu hadi tisa haruhusiwi kupanda bodaboda kwa ajili ya ya usalama wake.

"Lakini sasa siyo mtoto mmoja tu, wanapakiza watatu hadi wanne kwenye bodaboda moja... ni marufuku watoto wa umri huo kubebwa na bodaboda," alionya.

Ofisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji wa Muheza, Johari Mtango, alisema usafirishaji holela wa wanafunzi ni hatari kwa kuwa hata akipata ajali hatalipwa fidia kwa kuwa mabasi wanayotumia hawana mkataba nao.



Meneja wa kituo cha vijana walioathirika na dawa za kulevya wa Mchakamkacha Recovering Centre (MRC) cha kata ya Karanga, Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, Bazil Ngotty (kulia), akitoa elimu ya namna ya kuachana na matumizi ya dawa hizo kwa baadhi ya vijana waraibu wanaoendelea na matibabu ya kuachana nayo, kituoni hapo juzi. **PICHA: JAMES LANKA**

# Milioni 400/- kuondoa kero ya maji

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WIZARA ya Maji imeipatia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi (MUWSA) Sh. milioni 400 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa uboreshaji huduma za maji katika mji mdogo wa Himo wilayani hapa.

Baada ya kukabidhiwa kiasi hicho, MUWSA imeanza kulaza mabomba yenye urefu wa kilomita 33 katika kata mbili za mji huo.

Katika mkutano wa hadhara uliofanyika juzi Kata ya Njia Panda, Amina Rashid, mkazi wa Kitongoji cha Otomoro, alisema kuwa kipindi cha nyuma walikuwa wakipata maji safi na salama mara moja kwa wiki, lakini baada ya kuingia MUWSA, huduma hiyo imeboreshwa kwa kuwapo maji ya uhakika. "Tunaishukuru serikali kututua ndoo kichwani kwa vitendo kwani tulikuwa tunateseka sana, tatizo la maji katika eneo letu la Njia Panda limekuwa historia," alisema Amina.

Mkazi mwingine, Juma Hamisi, alisema awali walikuwa wanatumia gharama kubwa kuunganishiwa huduma ya maji kutokana na miundombinu kuwa mbali na makazi yao, hivyo mradi huo wa uboreshaji huduma utawarahishia kupata huduma hiyo.

Mhandisi wa MUWSA, Deoglas Lyimo, alisema fedha hizo watalaza mtandao wa mabomba kilomita 33 kwa mji huo wenye kata za Makuyuni kilomita 18 na Njia Panda kilomita 15.

Lyimo aliwataka wakazi hao kuwa wavumilivu wakati mamlaka hiyo ikiendelea kuboresha huduma ya maji kwenye maeneo yao.

"Kipindi cha nyuma wananchi walikuwa wakivuta maji kutoka umbali mrefu na kupelekea wakati mwingine mabomba kuziba na kutoboka.

"Tangu MUWSA tukabidhiwe tumeendelea kuboresha mtandao wa zamani na kuweka mpya ambao unapita karibu na makazi yao ili iwe nafuu kwa kuunganishiwa huduma," alisema.

Aliwataka kulinda miundombinu hiyo kwa kuwa serikali inatumia fedha nyingi na kuwataka kuwafichua wanaohujumu mamlaka hiyo na kuharibu miundombinu kwa makusudi.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

## MADILI YA WATOTO ZAMANI

# Kiti cha baba hakikaliwi, kusikiliza redio hadi arudi

**Na Adam Fungamwango**

NAKUMBUKA katikati ya miaka ya 1980, nikiwa Mpanda mkoani Rukwa (sasa Katavi) wakati huo kabla ya kuitwa Katavi.

Ulifika wakati wa kula. Tukaitwa watoto wote kwenda kupata chakula cha mchana. Chakula kiliwekwa kwenye kigoda na vigoda vingine vichache vikiwa pembeni.

Nilikuwa sielewi utamaduni au taratibu za huko kwa sababu ilikuwa ndiyo siku ya kwanza kufika huko na mama yangu tukitokea Dar es Salaam, kwenda kusalimia.

Watoto wenzangu wote walikaa chini. Wakanawa na kuanza kula. Babu yangu mzaa mama na mwenzake mmoja wakakaa kwenye vigoda. Mimi kwa sababu sielewi kitu nikavuta kigoda kimoja na kukaa.

Kilichotokea ni kwamba babu alinifokea na kunitaka nikae chini mara moja. Nikatoka kwenye kigoda haraka na kukaa chini.

"Mambo ya kwenu mjini usiyalete hapa. Hapa watoto wanakaa chini na watu wazima ndiyo wanakaa kwenye vigoda. Hizo ndizo taratibu za kwetu. Mtoto hawezi kukaa kwenye kigoda awe sawa na mtu mzima." Babu akanifafanulia.

Tangu siku hiyo nikawa natii amri bila shuruti, hadi niliporejea Dar es Salaam na mama.

Hii ilionyesha kuwa zamani kulikuwa na aina fulani ya maisha, utamaduni na taratibu zilizoendana na sehemu na mazingira. Baadhi zilitofautiana na zingine zilifanana.

Mimi nilizoea mjini tunakula tukiwa tumekaa kwenye viti, wakubwa na wadogo. Mara chache sana ndiyo chini na hasa tukila na akinamama. Kwenye viti ni wakati wa kula na baba, au wageni.

Hata hivyo, bado akinababa walikuwa na viti vyao. Hivi ni vile vya kupumzikia nje wakati wanapunga hewa, au wanapumzika.

Vingi vilikuwa vinatengenezwa kwa mbao. Kuna vya kukunja na vile ambavyo wenyewe wanaviita 'viti vya uvivu'.

Ni viti ambavyo vilikuwa vinatumiwa na kinababa peke yao. Hata kwa bahati mbaya, huwezi kukuta hata mama ameamua kukikalia, achilia mbali mtoto.


Tayari yalishatengenezwa mazingira kuwa ni kiti cha baba, hivyo watoto pamoja na utundu wao wote, hawakuvigusa.

Na ikitokea bahati mbaya ikawa hivyo, adhabu yake ni viboko.

Wazazi wa zamani walikuwa hawamnyimi mtoto viboko. Kosa la kujirudiarudia, liliweza kusababisha kucharazwa bakora kila siku.

Viti hivi vilitumiwa kina baba wanaporudi kazini, anatoka nacho kwenda nje, kwenye kivuli, upepo na tulivu, anakuwa amevaa kaptura au msuli wake, juu ana 'singlendi', mawani ya macho na gazeti lake, atakaa hapo hadi atapochoka, au kuitwa ndani kwenda kula chakula.

Wakati mwingine anaweza kuwa amepiga suti yake au shati na tai amekaa sebuleni, hapo kila mtoto kama alikuwa nje anahofia kuingia ndani kwani atakutana naye na maswali yataanza.



Huyu ndiyo baba wa zamani, watoto wa sasa wanamwita 'mdingi', yaani amekaa kinokonoko kabisa. Amekaa kwenye kiti cha uvivu sebuleni na kikaratasi chake, macho akiangalia mlangoni nani anapita, hapo watoto wote wanaogopa kupita kwenda ndani. Sasa jichanganye tu hapo, uone shughuli yake, fimbo zitakuhusu na utakwenda kuchuma mwenyewe.



Aina ya kiti ambacho kilikuwa kinatumiwa au kupendwa sana na akinababa wa zamani, ambavyo walipenda sana kukalia wakiwa barazani, nje ya nyumba, au sebuleni wakiwa wamepumzika.

Mzee hapo macho yake yanakuwa 'kinoko' tu, (tazama picha ya dingi hapo), ukiingia unaweza kuambiwa kalete madaftari, sasa akute makosa, halafu pia unaweza kutumwa kazi yoyote ile. Kinababa wa zamani walikuwa hawapendi kukuta watoto wao wamekaa tu bila kazi yoyote.

Atabuni au kuangalia mapungufu yoyote ndani mle ili awape kazi ya kufanya.

Ndiyo maana watoto za wa zamani akimuona baba amekaa sebuleni, anajiuliza mara mbili mbili, maana unahofia kuitwa na kuanza kuulizwa maswali ambayo yanaweza kukutia hatiani.

Wakati watoto wa sasa wanakaa sebuleni wakiwa wana uhuru wa kuchagua chaneli yoyote ya televisheni na kuangalia hata wazazi wao wakiwepo, zamani haikuwa hivyo.

Redio yenyewe kusikiliza hadi baba awepo. Kitendo chochote cha kutafuta redio ilipo na kuifungulia mwenyewe hayupo ni kosa kubwa ambalo linaweza kusababisha adhabu ya viboko.

Halafu walikuwa na uwezo wa kuweka sehemu ambayo hata ukiishika tu na kuangalia, ukairudisha tena akirudi anajua kuwa kuna mtu ameigusa redio yake. Na hadi mtasema ni nani.

Yoyote anayetaka kusikiliza redio ni lazima amsubiri baba arudi, afungilie ndipo watoto mkae msikilize. Na hata kusikiliza kwenyewe si vipindi vyote. Kuna vipindi ambavyo watoto wanaambiwa waondoke kwani haviwahusu.

Wapo watoto waliokuwa watundu zaidi ambao walikuwa na uwezo wa kufungua, kusikiliza na kurudisha bila baba kujua.

Hapo sasa kuna kuzidiana akili, kati ya baba na mtoto.

Ukimkuta baba mwingine akiona betri zinaisha wakati hajatumia kwa muda mrefu, anaanza kuhisi kuna mtu huwa anafungulia redio yake.

Atakachofanya ni kuzigeuza betri. Kama redio ya betri nne, kati ya kati itageuzwa ielekee upande mwingine, hivyo yoyote atayeifungua itaendelea kunyamaza tu.

Ni udadisi wa hali ya juu tu ndiyo unaweza kugundua kuwa betri moja imegeuzwa, vinginevyo unaiacha na kuendelea na shughuli zako.

Hii haikuwa na maana kuwa wazazi wa zamani walikuwa na roho mbaya na hawapendi watoto wao, la hasha.

Ilikuwa ni kuwajenga kwenye utamaduni wa nidhamu na adabu.

Pia ikumbukwe kipindi hicho waliokuwa na redio ni wachache, na si wengi waliokuwa na uwezo wa kuimiliki.

Kwa sababu hiyo ilikuwa ni kama kuilinda ili watoto wasiharibu. Hata upatikanaji wa betri nao ulikuwa ni wa mbinde.

Unaweza kuwa na redio, lakini uweze kupata betri hata miezi miwili.

Baba akaishia tu kubondabonda betri zilizopo na kuzianika juani, ili redio ipate kuongea hata kwa dakika 30 tu.

Ndugu msomaji unaweza kutuandikia moja ya maadili ya zamani kwa watoto unayoyafahamu au kukutana nayo.

**Tuma meseji 0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

## Mafuriko yaua 50 Kenya

**NAIROBI,** KENYA

WATU 50 wamefariki dunia nchini Kenya baada ya mafuriko kuyakumba maeneo mbalimbali kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Taarifa zilisema kaunti ya Mombasa na Tana River ni baadhi ya majimbo yalioathirika na mafuriko hayo.

Shirika la msalaba mwekundu nchini humo lilisema familia 156 katika eneo la Bandi katika eneo la Garsen katika kaunti ya Tana River Kaskazini Mashariki wamehama makazi yao baada ya nyumba zao kufunikwa na maji.

Aidha inahofiwa idadi huenda ikaongezeka kutokana na mvua zaidi ya wastani zinazoendelea kunyesha.

Kwa mujibu wa baadhi ya video zilizosambazwa na shirika hilo la vyombo vya habari vya ndani, zilionyesha nyumba zikiwa zimejaa maji katika kaunti ya Mombasa.

Ripoti kutoka kwa shirika la msalaba mwekundu zinaeleza kuwa watu 52 wamefariki kutokana na mafuriko, wakati wengine 24,415 wakipoteza makazi yao katika maeneo tofauti ya nchi.

Mkoa wa bonde la ufa umeripoti vifo vya watu 15 na wengine watatu wamejeruhiwa.

Taarifa hiyo ilisema watu 1,657 wamehama makazi yao kutokana na mafuriko yanayosababishwa na mvua kubwa inayoendelea.

Katika eneo la Nyanza, watu sita wameripotiwa kufariki na wengine 116 wakipoteza makazi yao.

Huko Magharibi mwa Kenya, watu wanne wameripotiwa kufariki, wanne wakijeruhiwa na 154 wamekimbia nyumba zao.

Idara ya utabiri wa hali ya hewa imeonya kuwa mvua inayoshuhudiwa kwenye taifa hilo itaendelea hadi mwezi Januari mwaka wa 2024.

**RFI**

## George Weah mambo magumu

**MONROVIA,** LIBERIA

Kiongozi wa upinzani nchini Liberia Joseph Boakai anaongoza kwa asilimia 50.58 dhidi ya Rais George Weah ambaye amepata 49.42.

Katika matokeo ya duru ya pili yanayotolewa na Tume ya Uchaguzi nchini humo inaonyesha George Weah ambaye ni mwanasoka maarufu anaweza kushindwa kama matokeo hayo yataendelea kumbeba mpinzani wake.

Tayari asilimia tisini ya kura zimeshahesabiwa na tume ya uchaguzi nchini humo.

Katika duru ya kwanza ya kura, wagombea hao walishindwa kupata zaidi ya asilimia hamsini ya kura.

Katika duru hii ya pili, mshindi atakayepata kura nyingi ndiye atatangazwa mshindi.

Rais Weah anatafuta muhula wa pili kusalia madarakani akiahidi kuboresha elimu,ajira na kukabiliana na ufisadi. Boakai kwa pande wake ameahidi kuinusuru Liberia kutoka kwenye uongozi mbovu na usimamizi mbaya wa rasilimali za nchi unaofanywa na Weah.

**BBC**

# Israel yakiri haikufanikiwa kupunguza vifo kwa raia Gaza

**TEL AVIV,** ISRAEL

SERIKALI ya Israel imekiri kwamba imeshindwa kupunguza vifo vya raia wasio na hatia katika vita inayoendelea katika Ukanda wa Gaza.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu alisema juzi kwamba juhudi za vikosi vyake kupunguza vifo vya raia hazikufanikiwa, na kuilaumu Hamas kwa kuanzisha vita hivyo.

Netanyahu alisema jeshi la Israel linafanya kila iwezalo kuitokomeza Hamas, lakini kundi hilo linatumia raia kama ngao.

"Jambo lingine ninaloweza kusema ni kwamba tutajaribu kumaliza kazi hiyo na majeruhi wachache wa raia. Hilo ndilo tunalojaribu kufanya, kupata majeruhi wachache kwa raia, lakini kwa bahati mbaya, hatujafanikiwa." Alisema.

Aidha, Benjamin Netanyahu alisema walivamia hospitali ya Al Shifa baada ya kuwepo na uwezekano mkubwa wa kuwepo kwa mateka wanaoshikiliwa na Hamas ndani ya hospitali hiyo iliyoko mjini Gaza.

"Ilikuwa sababu mojawapo iliyotufanya tuingie hospitalini, alisema katika mahojiano na televisheni ya CBS katika kipindi cha Evening News. Israel imewashutumu Hamas mara kwa mara kwa kuwa na kambi chini ya hospitali ya Al-Shifa jambo ambalo Hamas ilikanusha.

Vikosi vya Israel vilivamia hospitali ya Al Shifa siku ya Jumatano, lakini Netanyahu alisema walipofika, mateka hawakuwapo.

"Kama walikuwa mateka ndani, walitolewa nje, serikali ina intelijensia kuhusu mateka kuwepo," alisisitiza.

Awali, jeshi la Israel lilisema limepata mwili wa mwanamke ambaye alikuwa miongoni mwa mateka wanaoshikiliwa na wanamgambo wa Hamas karibu na hospitali ya Al Shifa.

Jeshi hilo limesema walimpata Yehudit Weiss akiwa ameuawa walipokuwa wakifanya opresheni yao ndani ya Al Shifa, lakini hawakutoa maelezo zaidi.

Wakati hayo yakijiri, mkuu wa hospitali hiyo Muhammud Abu Salmiya, alisema wanakabiliwa na janga baya baada ya kuishiwa maji na gesi ya Oksijeni.

Alisema ndani ya hospitali hiyo kuna wagonjwa 650,wahudumu mia tano na takriban watu elfu tano waliotafuta hifadhi ndani ya hospitali hiyo. Mawasiliano ya simu na intaneti yamezimwa katika Ukanda wa Gaza kwa sababu ya ukosefu wa mafuta.

Tamara Al-Rifai, ambaye ni mfanyakazi wa shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia wakimbizi wa Palestina (UNRWA) aliambia BBC kuwa kutatizwa huko kwa mawasiliano kutawaathiri watu wa Gaza.

Wakati huo huo, Jeshi la Israel lilitoa taarifa ya kuwaua watu watano wenye silaha katika mapigano yaliyofanyika usiku kucha wa jana.

Aidha saa chache lilichapisha picha na video kwenye ukurasa wa X, ambazo wanadai zinaonyesha mahandaki ya Hamas chini ya hospitali zilizoko Gaza.

BBC haikuweza kuthibitisha picha hizo kama halisi au zimetengenezwa.

"Handaki la magaidi wa Hamas limepatikana ndani ya jengo la Hospitali ya Shifa," ilisema IDF katika taarifa iliyoambatana na video ambayo walidai ilionyesha lango la njia ya chini kwa chini katika uwanja wa hospitali hiyo.

**BBC**



Mwanajeshi wa Israel akiangalia majengo yaliyoharibiwa Ukanda wa Gaza wakati wa mapambano na Hamas jana. **PICHA: IDF**

## Sudan yaomba walinda amani waondoke

**KHARTOUM,** SUDAN

SUDAN imetoa wito wa kuondolewa kwa ujumbe wa kulinda amani wa Umoja wa Mataifa (UNITAMS) katika taifa hilo.

Hata hivyo, serikali ya kijeshi ya nchi hiyo ilisema bado imejitolea kushirikiana na Umoja wa Mataifa.

Kupitia barua waliyomuandikia Katibu Mkuu wa umoja huo Antonio Guterres, na pia katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, kaimu waziri wa mambo ya nje wa nchi hiyo Ali Sadeq, alitaka wafanyakazi hao waondolewe mara moja.

Sadeq alisema madhumuni ya kuanzisha misheni hiyo ilikuwa kusaidia serikali ya mpito ya Sudan baada ya mapinduzi ya Desemba 2018, lakini utendaji kazi wa ujumbe huo katika kutekeleza malengo yake umekuwa wa kukatisha tamaa.

Ujumbe huo una zaidi ya wafanyakazi 400 wengi wao wakiwa ni raia.

**BBC**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA SINGIDA**
**LILILOPO SINGIDA**
**SHAURI LA MAOMBI MADOGO YA ARDHI NA. 123 YA 2022**
**ISSA SHABANI............MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**ASHA ALLY NGAA............MJIBU MAOMBI**

**KWA: ASHA ALLY NGAA**
**POPOTE ULIPO TANZANIA**

### KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa mwombaji tajwa hapo juu ameleta maombi yake hapa Barazani ambayo maelekezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi, ambayo yanaweza kupatikana katika Baraza hili , kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria hapa Barazani tarehe 17/11/2023 saa 2:00 asubuhi siku ya kutajwa kwa shauri hilo.

Unatakiwa uhudhurie mwenyewe au mwakilishi wako anaetambua kisheria siku na saa tajwa hapo juu.

ANGALIA: Kushindwa au kupuuza kufika tarehe na saa iliyotajwa hapo juu kesi itapangwa na kusikilizwa upande moja tu na uamuzi kutolewa bila ya wewe au mwakilishi wako kuwepo.

HATI hii imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya BARAZA hii leo tarehe 06 Mwezi wa November, Mwaka 2023

---

**IN THE DISTRICT COURT OF ILALA**
**ATA SAMORA AVENUE**
**CIVIL CASE NO. 08/2023**
**BANK OF AFRICA TANZANIA LTD...........PLAINTIFF**
**VERSUS**
**PETER ALPHONCE DINDILI.................DEFENDANT**
**TO: PETER ALPHONCE DINDILI**
**P.O. Box 20950**
**DAR ES SALAAM.**

Take notice that the Plaintiff has instituted a suit against you with particulars of claim set out in a plaint filed in this court. Service of the summons on you has been ordered by means of this publication. You are defected to collect copies of the summons and plaint from the court's registry.

You are hereby summoned to appear in this court in person or by an advocate or an agent duly authorized on 4/12/2023 at 8:30 a.m when this suit will be mentioned.

Take further notice that should you default to enter appearance in court on the day time mentioned above, the suit will proceed and judgment may be given in your absence.

Given under my hand and the seal of the court this day of 16/11/2023.

RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT ILALA
DAR ES SALAAM

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya CHAMWINO MJINI DODOMA**
**Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo Cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai/Ndoa Na.86/2023**
**JINA LA MDAI...........MAGDALENA MAKINDI**
**JINA LA MDAIWA..........GASPA PAULO**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 27 mwezi 11 mwaka 2023 saa 02:30 asubuhi kwa mujibu wa Madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini.Mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa Kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 16 mwezi 11 mwaka 2

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**VAILET A SIMBOWE,** Anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha Nne chenye Index no S2066-0032 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya **IPUNGA SEKONDARI** Mwaka 2015 Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**TAARIFA YA POLISI: CONTROL NO 9910839157038**

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(COMMERCIAL DIVISION)**
**AT ARUSHA**
**MISCELLANEOUS COMMERCIAL APPLICANT NO. 12 OF 2023**
**STEPHEN MAHENDEKA MGANGA.....APPLICANT/DECREE HOLDER**
**VERSUS**
**BEST WAY CAPITAL MANAGEMENT LIMITED**
**(BCM)..........RESPONDENT/JUDGEMENT DEBTOR**
**SUBSTITUTED SERVICE BY PUBLICATION**

**TO:**
**Managing Director,**
**Best way Capital Management Limited,**
**P.O.Box 1053395**
**DAR ES SALAAM.**

**TAKE NOTICE** that the Applicant has instituted a suit against you with particulars of claim set out in the application filed in this Court.

Service of the Summons on you has been ordered by means of this publication. You are directed to collect copies of the summons and application from the Court's Registry , P.O. Box 3140 Arusha.

You are hereby summoned to appear in this Court in person or by an Advocate or an agent duly authorized on 30th day of November,2023 at 12:00 hours when this case will be mentioned.

**TAKE FURTHER NOTICE** that, should you default to enter appearance in Court on the day and time mentioned above, the case will proceed and ruling may be given in your absence.

Given under my Hand and the Seal of the Court this 15th day of November ,2023

DEPUTY REGISTRAR
ARUSHA

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MOHAMMED ENTERPRISES (T) LTD**

inatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba ya usajili MC 532 CVC aina ya BOXER. Chassis namba MDZAZ1BX9LWJ90634. Engine namba PFXWLJ03169. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/9069/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI /TARAKA/MIRATHI NAMBA 199/2023**
**MDAI/MUOMBAJI/MSIMAMIZI: SHEDRACK BAKARI**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: SOILA PUBLIC LIMITED**

**KWA: SOILA PUBLIC LIMITED**

**OMBI LA MDAI : MADAI NO.199/2023**
**MADAI YA PESA TSH.2,400,000/=**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri lilimepangawa kusikilizwa mnamo tarehe 20 Mwezi 11 Mwaka 2023 saa 2:30 Asubuhi .

Angalia kama hukudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii inaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 16/11/2023

.............................................
**HAKIMU**
**MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**MOROGORO**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SUZAN KUNDI JILALA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA PASSO yenye usajili namba T 390 DVY, CHASSIS NAMBA: KGC100229514 na ENGINE NAMBA: 1KR0717534. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/36824/2023**

---

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

## MAMA MWENYE NYUMBA - 2

MWANTUMU, au mama Mwadawa, ni mwanamke ambaye muda wote yeye anachowaza ni umbea, ugomvi na kufitinisha watu. Anawagombanisha majirani wasielewane, ndoa za majirani zake nazo haziko salama hajaziacha, kwani amekuwa akizitikisa. Kwa bahati mbaya au nzuri anaishi kwenye nyumba ya urithi ya marehemu mama yake, yeye akiwa ndiye mama mwenye nyumba. Cheo hicho cha umama wa nyumba asiyojenga, ndiyo akawa sasa amepata fimbo ya kuwapigia watu. Wapangaji wanaopanga kwenye nyumba hiyo wamekuwa wakiishi kwa amri, manyanyaso, kufokewa kama watoto wadogo. Ndani ya nyumba hiyo, wapangaji wamekuwa wakiishi bure na mama wa kambo, huku silaha yake kubwa ikiwa ni kuwatishia kuwahamisha. Hebu fuatilia mwanzo hadi mwisho wa visa vya mama huyu.

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Tabia ni kama ngozi ya goti, haibadiliki. Ameendelea kuwa na tabia ile ile. Hata akipata pesa za kodi anashindwa kukarabati nyumba ambayo kila siku zinavyozidi kwenda inaendelea kuwa mbovu.

Mdogo wake Tatu analalamika kuwa hapewi pesa za kodi, badala yake dada yake anakula mwenyewe.

Mwantumu hampi pesa mdogo wake kwa sababu tu eti mumewe ana uwezo.

Anapopata pesa zake, atakwenda kununua kila kitu kizuri anachokiona, nguo, chakula kizuri, lakini jioni atakusanya shoga zake kwenda baa kunywa.

Zikiisha anafanya kazi ya kuombaomba na kuwasumbua wapangaji wake wa kiume wamkopeshe pesa.

Mwantumu ana watoto wawili wasichana ambao kila mmoja alizaa na baba tofauti.

Wote baada ya kumaliza kidato cha nne wapo nyumbani, na wamerudi kuishi hapo na mama yao.

Mabinti hao wawili ni Amina na Anifa.

**********************************


“Baba nakwambia, mimi sina ugomvi na wewe, lakini yule mke wako anaweza kusababisha nikawahamisha kabisa ndani mle.”

“Mama tusamehe, unajua tena ukinihamisha sijui itakuwaje. Maana hapa mjini tatizo siyo pesa. Ila bajeti ya kuhama, kulipa pesa ya kuingia nyumba nyingine, halafu huwezi kujua nyumba unayohamia, zingine siyo nyumba...”

“Kama ulikuwepo. Nyingine mauzauza tu. Sasa mkeo ndiyo anataka kukupeleka. Usiku mkilala mara mmetokewa na mazombi, mara mnacharazwa bakora bila kumuona mtu anayewapiga wakati mwingine riziki haipatikani.”

“Ndiyo mama naona kabisa tangu nihamie hapa miaka miwili iliyopita angalau nimepiga kidogo hatua, nilikuwa na televisheni ya chogo, sasa hivi nina flati, tusamehe bure tutafanyaje ndiyo wake wetu hawa.”

Ni maongezi na Mwantumu na mpangaji wake Jonas, mume wa Devota. Hakufanyika nyumbani. Mwantumu alimvizia Jonas anaondoka na yeye akamfuata nyuma nyuma hadi maeneo ya Magomeni Ndugumbi, karibu kabisa na Uwanja wa Barafu.




**“Siyo hivyo vipi wakati ulikuja mwenyewe nyumbani kuazima taiti, gauni na blauzi nimekupa, hadi leo hujarudisha?”**

Mahesabu ya Mwantumu aliona hapo hapatakuwa na watu wanaomfahamu ambao watapeleka umbea kwa mkewe.

“Mkeo ananitolea mimi mineno ya shombo. Mkeo hataki kufanya usafi, kweli. Nikisema mtasema mwenye nyumba ana mdomo.”

“Hapana mama, tusamehe, si unajua wanawake wetu hawa wa kiswahili?”

Mwantumu akageuka huku na huku, kama vile anahofia mtu asiwasikie, halafu akamsogelea karibu kama hatua moja, akaongea kwa sauti ya uangalifu kidogo, akiwa amepunguza ile ya mwanzo.

“Na mwanamke yule wewe umemuokota wapi? Mwanaume mzuri, mtanashati kama wewe na kwenda kuwa na kijanamke chenyewe chembamba kama kinakula simenti, chini miguu kama fito za kujengea nyumba ya udongo, haya mtu mwembamba, lakini miziwa mama miziwa, he we baba...”

“Mama Devota hawakuwa hivi, alikuwa mrembo sema tu nadhani maisha tu...”

“Ndiyo bwana wewe, sasa hivi kwa jinsi ulivyo unatakiwa uwe na japo mwanamke mwingine pembeni akupetipeti.”

“Mhh, kweli mama?” Jonas akaonekana kunogewa na mazungumzo mama mwenye nyumba wake.

“Ohoo! Kalagabalo, Mzaramo kalonga.”

Jonas alikuwa na tabia ya kupenda wasichana. Hakuwa mwaminifu kwa asilimia mia mia moja.

Kauli ya kuambiwa atapata demu wa pembeni ilimfurahisha, japo hakutaka kuiweka bayana.

Alimfahamu mama mwenye nyumba wake ni mama wa mjini, hivyo anaweza kumpatia msichana mwingine mrembo.

“Enhee nani tena huyo?”

“Nani mwingine kama siyo Amina.”

“Amina binti yako?” Jonas akashangaa.

“Ndiyo, binti mbichi kama yule atakuwa sawa na limama lako lile.”

Jonas hakutegemea jibu lile, lilimshangaza, lakini akafurahi kimoyomoyo.

Amina amemaliza kidato cha nne na kufeli kwenda la tano. Amejifunza urembo na sasa anafanya kazi saluni.

Wajihi wake ni mwembamba mrefu, lakini umbile lake limekaa kimisi zaidi, mweupe na mwenye kupenda kuvaa mavazi ya kisasa.

Mate yakamtoka Jonas na akamjibu mama mwenye nyumba wake, “Basi mama fanya unavyoona inafaa.”

“We niachie hilo, usikonde kabisa.”

Waliachana, Jonas akiwa anaelekea kibaruani, na mama mwenye nyumba anarejea kwake.

“Enhee wee bibi bora nimekuona.” Ilikuwa ni sauti iliyomshtua ya mwanamke aliyekuwa anamfuata nyuma yake ambaye awali hakumuona.

“Leo nimekutokea kwa nyuma, nimekusubiri kwanza upite, maana kila ukiniona unanikimbia.”

“Nakukimbia vipi Bishada?”

“Yaani kukutendea wema malipo yake ndiyo haya?” Akahoji Bishada ambaye ni mmoja wa wakazi wa Magomeni Makuti.

Mwantumu ilibidi awe mpole zaidi, akajibu kwa upole ili watu wengi wasisikie.

“Hapana shoga siyo hivyo.”

“Siyo hivyo vipi wakati ulikuja mwenyewe nyumbani kuazima taiti, gauni na blauzi nimekupa, hadi leo hujarudisha?”

“Nisamehe mwenzangu, nimevurugwa na wapangaji wangu. Tuachane na hayo Bishada, unauona mguu huu, wa kwako huu!” Aliongea huku akiangalia mguu wake chini.

“Kuna nini tena mama Amina?”

“Kwanza nilitaka kukufuata nikupe taarifa ya shughuli shoga, miezi miwili ijayo, dada yangu Mkuranga anaozesha, halafu nikupe umbeya.”

“Umbeya wa nani tena?”

“Wako wewe mwenyewe. Wanavyokuongelea. Yaani shoga yangu ukiwa unaongea na watu, ukiwapa kisogo tu, wanakung’ong’a.”

“Mimi huyo?”

“Kwani kuna Bishada wawili? Si yupo mmoja tu ambaye ni wewe!”

“He, niambie koma!”

“Wanakuongelea vibaya dada yangu, yaani wewe hapo huna nguo.”

ITAENDELEA JUMAMOSI

## HABARI MICHEZO

# SHIME: TUNATAKA KUFUZU, TUPO IMARA

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuwasili salama Abuja, Nigeria, Kocha Mkuu wa timu ya soka ya Taifa ya Wanawake wenye umri chini ya miaka 20 'Tanzanite', Bakari Shime amesema kikosi chake kipo imara na wapo tayari kusaka ushindi katika mchezo wa marudiano wa kufuzu kombe la Dunia dhidi ya wenyeji wao Nigeria.

Tanzanite iliwasili Nigeria mapema juzi kwa ajili ya mchezo huo unaotarajiwa kuchezwa kesho baada ya mechi ya kwanza iliyochezwa uwanja wa Azam Complex wiki moja iliyopita kutoka sare ya bao 1-1.

Akizungumza na Nipashe jana, Shime alisema baada ya kuwasili wamefanya mazoezi mepesi ya Gym na jana walirejea katika uwanja wa mazoezi kufundisha mbinu kuelekea mchezo huo.

Alisema wamefanya maandalizi mazuri kwa ajili ya kutafuta ushindi au sare yenye faida kwao ambayo itawasogeza mbele katika hatua nyingine ya mashindano hayo ya kufuzu kombe la Dunia.

"Wachezaji wangu wapo tayari kwa mchezo huu, ninaamini tunaweza kufanya vizuri, tunahitaji matokeo mazuri yenye faida kwetu, nafahamu sare ya kuanzia mabao 2-2 itatufanya tusonge mbele na kufikia malengo yetu ya kwenda kucheza kucheza kombe la Dunia, lakini sisi tunataka ushindi" alisema Shime.

Wakati huo huo, Katibu Mtendaji wa Baraza la Michezo Taifa (BMT), Neema Msitha alisema wanafahamu Tanzanite wanauwezo wa kufanya vizuri kwenye mchezo huo licha ya mchezo wa awali kutoka sare ya bao 1-1 hapa nchini.

Alisema wamewaona wapinzani wao, ni wazuri, lakini Tanzania ina kikosi kuzuri sana na watanzani wanatakiwa kuisapoti timu yao iliyopo Nigeria kwa maombi ili ifanye vizuri.

"Nawaomba wachezaji wapambane, hii ni mechi muhimu sana kwetu, kama tutafanya vizuri katika mchezo huu basi nina imani timu yoyote itakayofuata kati Burundi au Congo tunaweza kuzifunga na kukata tiketi ya kwenda kucheza kombe la Dunia," alisema Neema.

UZINDUZI...




Naibu Kamishna wa Ubalozi wa India nchini Tanzania, Manoj Varma (katikati), akiwa pamoja na Waratibu wa mbio za kirafiki za nchi hizo mbili, Mahesh Joshi na Nikki Aggarwal wakibonyeza kitufe kuzindua mbio hizo jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mratibu wa matukio wa mbio hizo Taji Liundi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbio za urafiki, India-Tanzania zazinduliwa Dar

**Na Mwandishi Wetu**

MBIO za urafiki za umoja wa nchi za India na Tanzania zimezinduliwa rasmi jana na ubalozi wa India hapa nchini.

Mbio hizo za Marathon zimepangwa kufanyika Desemba 30 na 31 ambapo mwanariadha maarufu wa India Milind Soman atakimbia kilometa 120 kutoka Dar es Salaam mpaka Bagamoyo na kurudi.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam katika hafla fupi ya kuzindua mbio hizo, Naibu Kamishna Mkuu wa Ubalozi wa India nchini Tanzania, Manoj Varma, alisema watanzania wanakaribishwa kushiriki pamoja na Soman katika mbio hizo za siku mbili.

Alisema wameandaa mbio hizo kuhakikisha wanadumisha umoja uliopo kati ya nchi hizo mbili ikiwemo wanariadha mbalimbali kubadilishana mawazo.

"Litakuwa tukio la kipekee katika kudumisha umoja wa nchi hizi mbili marafiki, milango ipo wazi kwa watu wote kujiandikisha kushiriki," alisema Manoj.

Alisema Ubalozi wa India unayofuraha kuandaa mbio hizo na hiyo itakuwa njia moja wapo ya kuunga mkono juhudi za Rais wa Tanzania, Dk Samia Suluhu Hassan katika kuendeleza michezo na kudumisha ushirikiano wa kimataifa.

Aidha, Mratibu wa mbio hizo, Mahesh Joshi, alisema mbio hizo siku ya kwanza zitaanzia mitaa ya Dar es Salaam hadi Bagamoyo na siku ya pili zitaanzia Bagamoyo kurudi Dar es Salaam ambapo zitajumusha jumla ya kilometa 120.

"Umoja wa India na Tanzania tumeandaa mbio hizi ambapo kwa ujumla wake Soman na wakimbiaji wengine watakimbia jumla ya kilometa 120 kwa siku mbili," alisema Joshi.

Kwa upande wake, Soman aliwataka watanzania wengi kujitokeza kwenye mbizo hizo ambapo mbali na kudumisha umoja uliopo kati ya nchi hizo mbili lakini pia watajenga miili yao na kuboresha afya.

"Ni fursa nzuri kwetu kama wananchi marafiki, nasubiri kwa shauku kubwa kuungana na watanzania kukimbia mbio hizi, watu wajitokeze kwa wingi.

Alisema amefanya mbio kama hizo katika nchi nyingi Duniani na anjivunia na kuwa na furaha kuja kushiriki na wananchi wa Tanzania.

Mwanariadha huyo Mkongwe hii itakuwa mara ya pili kuja Tanzania ambapo mara ya kwanza alifanya hivyo miaka ya nyuma alipokuja kupanda Mlima Kilimanjaro.

# Serikali kuisapoti Pazi kikapu Afrika

**Na Saada Akida**

SERIKALI kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo imeahidi kuiunga mkono timu ya mpira wa kikapu ya Pazi inayokwenda Afrika Kusini kushiriki mashindano ya hatua ya 16 bora ya kufuzu fainali za Afrika za mchezo huo.

Aidha, Serikali imeuagiza Ubalozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini kuipokea timu hiyo na kuomba Watanzania walioko huko kuisapoti katika kipindi chote itakapokuwa kwenye mashindano hayo ya kufuzu yatakayoanza Novemba 21 mpaka 26.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana katika hafla fupi ya kuiaga timu hiyo, Waziri wa Wizara hiyo, Dk Damas Ndumbaro kwanza alimpongeza Rais wa timu hiyo, Mussa Mzenjii kwa kuonesha juhudi na kufika hatua ya 16 bora akisema wataiunga mkono ili waipeperushe vyema bendera ya Taifa.

"Tunaamini Pazi itafanya vizuri, tutawasiliana na Balozi wa Afrika Kusini ili awahimize Watanzania waipe sapoti kwa kipindi chote mtakachokuwa huko, waiunge mkono timu iweze kufanya vizuri,"alisema Waziri Ndumbaro na kuwatakia kila la heri.

Kwa upande wake Kocha Mkuu wa timu hiyo, Henry Mwinuka alisema timu itaondoka alfajiri ya leo kuelekea nchini humo kwa ajili ya kuianza kampeni ya kutafuta nafasi ya kushiriki fainali za Afrika.

Alisema mashindano hayo ya hatua ya 16 bora Tanzania ipo kundi A ikiwa na timu za Cape Town ya Afrika Kusini, Dynamos ya Zambia na Shule ya NBA.

Alisema washindi wawili wa kundi hilo wataingia hatua ya nusu fainali na kukutana na timu mbili za kundi B, kutafuta washindi watatu watakaoungana na timu tisa zilizofuzu kwa ajili ya fainali hizo.

Mchezaji wa Pazi, Hasheem Thabeet alisema malengo yao ni kuhakikisha wanafanya vizuri katika hatua hiyo ili kusonga mbele hatua inayofuata na kuwaomba Watanzania kuendelea kuwaunga mkono wakaipeperushe vyema bendera ya Taifa.



## ZISIKUPITE

**TONEY KUJIFUNGA BRENTFORD**
KLABU ya Brentford ina imani kuwa mshambuliaji wa England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 27 ambaye amekuwa akihusishwa na Arsenal na Chelsea, atasaini mkataba mpya na klabu hiyo. (*Talksport*)

**SANE AWINDWA ENGLAND**
KLABU ya Manchester City itamenyana na Liverpool kumsajili tena mshambuliaji wa Bayern Munich na Ujerumani, Leroy Sane mwenye umri wa miaka 27. (*Bild, via Sun*)

**SIR RATCLIFFE NA MAN**
SIR Jim Ratcliffe, ambaye anakaribia kununua asilimia 25 ya Manchester United, anatarajiwa kuchukua mwongozo kutoka kwa Sir Alex Ferguson wakati akifanyia marekebisho klabu hiyo. (*Telegraph*)

**WERNER AZIVUTIA MBILI EPL**
KLABU ya Crystal Palace na Fulham zinavutiwa na mkataba wa mkopo wa mshambuliaji wa RB Leipzig na Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 27, ambaye amekosa namba katika klabu hiyo ya Bundesliga. (*90 min*)

**WAKALA WA GUNDOGAN APUUZA**
WAKALA wa kiungo wa Barcelona, Ilkay Gundogan amepuuzia mbali tetesi zinazomhusisha mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 33 na kuhamia klabu ya Uturuki ya Galatasaray. (*Mundo Deportivo*)

**KIWIOR KUONDOKA ARSENAL**
ARSENAL iko tayari kumruhusu mlinzi wa Poland, Jakub Kiwior kuondoka katika klabu hiyo kwa mkopo kwani mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 anataka muda zaidi wa kucheza katika kikosi cha kwanza. (*90 min*)

**SANTOS KUREJESHWA**
CHELSEA huenda wakamrejesha kiungo wa Brazil Andrey Santos mwenye umri wa miaka 19 kutoka klabu ya Nottingham Forest ambako anacheza kwa mkopo kwa sababu ya kukosa muda wa kucheza. (*Standard*)


**SO APUUZIA UZUSHI**
MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur, Son Heung-min mwenye umri wa miaka 31 amepuuza madai kwamba alipata jeraha alipokuwa akiichezea Korea Kusini katika mechi ya kufuzu kwa Kombe la Dunia 2026 dhidi ya Singapore. (*Standard*)

**GERMAN KUTUA MAN CITY**
KLABU ya Manchester City imekubali mkataba wa pauni milioni 1.2 kumsajili kiungo mshambuliaji wa Leeds United mwenye umri wa miaka 15 Finley Gorman. (*Football Insider*)

**ARSENAL NA RAYA**
ARSENAL ilizipiku Tottenham, Bayern Munich, Chelsea na Manchester United kumsajili mlinda mlango wa Hispania, David Raya mwenye umri wa miaka 28 kwa mkopo kutoka Brentford, kwa mujibu wa wakala wa mchezaji huyo. (*Metro*)

**ROBINSON AFUATILIWA**
KLABU za Aston Villa na Southampton zinamfuatilia kiungo wa Derby County mwenye umri wa miaka 18 kutoka Ireland Kaskazini, Darren Robinson. (*Football Insider*)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SANCHO ASHIKILIA MSIMAMO WAKE WA KUTOOMBA RADHI

**Muingereza huyo amedai kocha huyo amemtumia kama kichaka cha kujificha baada ya...**

**MANCHESTER,** England

WINGA wa Manchester United, Jadon Sancho inaelezwa ameshikilia msimamo wake wa kutotaka kuomba msamaha kwa kocha wa klabu hiyo, Erik Ten Hag.

**Sancho alitofautiana na Ten Hag baada ya kocha huyo kusema mchezaji huyo hakuonesha kiwango kizuri mazoezini kuelekea mchezo wa ligi kuu ya England dhidi ya Arsenal na ikawa sababu ya mchezaji huyo kutokucheza mchezo huo.**

Mchezaji huyo alikuja na andiko ambalo alilichapisha katika mtandao wake wa kijamii wa X zamani (Twitter) akieleza kuwa kocha huyo amemtumia kama kichaka cha kujifichia baada ya kupoteza mchezo huo dhidi ya Arsenal.

Baada ya kutofautia na kocha wake mchezaji huyo alipewa sharti moja la kuomba radhi kwa kocha huyo mbele ya wachezaji wenzake.

Lakini winga huyo amegoma kuomba radhi licha ya kushauriwa na na baadhi ya viongozi klabuni hapo na hata baadhi ya wachezaji wenzake.

Kwa mujibu wa ESPN, Sancho ameweka wazi kwamba, hawezi kuomba msamaha kwa sababu hakuna kosa alilolifanya.

Baada ya kuelezwa kuwa Sancho hana mpango wa kuomba msamaha kwa Hag ili arudi ndani ya timu hiyo, ni wazi mchezaji huyo yuko mbioni kuachana na klabu hiyo katika dirisha dogo la mwezi Januari.

# SON AWATOA HOFU MASHABIKI TOTTENHAM SPURS



**LONDON,** England

WINGA wa Klabu ya Tottenham Hotspurs, Heung Ming Son amewatoa hofu mashabiki baada ya kuonekana ameumia alipokua anaitumikia timu yake ya taifa ya Korea Kusini.

Son alionekana kuchechemea katika mchezo kati ya timu yake ya taifa dhidi ya Singapore.

Lakini baada ya mchezo huo Son amewatoa hofu mashabiki baada ya kusema hakuumia na yupo sawa.

Hofu ilianza kutanda kwa mashabiki wa klabu ya Tottenham baada ya kuona mchezaji huyo ni kama ameumia kwenye mchezo huo, jambo ambalo limefanya Son kuwatoa hofu mashabiki.

Tottenham kwa sasa inaaandamwa na majeraha ya wachezaji wake muhimu, hivyo kama nahodha wao huyo angeongezeka ingekua taarifa mbaya zaidi kwa klabu hiyo chini ya kocha Ange Postecoglou.

Son aliiongoza timu yake ya taifa ya Korea kupata ushindi wa mabao 5-0 mbele ya Singapore, huku yeye pia akifunga goli moja kati ya mabao hayo matano.

# *Baba afichua kuhusu Ramsdale*

**LONDON,** England

BABA wa golikipa Arsenal, Aaron Ramsdale amedai mtoto wake hana furaha na amepoteza tabasamu lake kwani klabu hiyo imemtosa chini ya kocha Mikel Arteta.

Kipa huyo wa zamani wa Sheffield United na Bournemouth mwenye umri wa miaka 25, aliwasili Emirates mwaka 2021 na moja kwa moja akaingizwa kwenye kikosi cha kwanza lakini sasa ameanza kusugua benchi tangu Septemba mwaka huu.




Kipa mpya aliyesajiliwa na Arteta kwa mkopo David Raya, ndiye amechukua nafasi ya Ramsdale tangu Septemba kwenye ushindi dhidi ya Everton.

Raya ambaye ni raia wa Hispania kwa sasa amekuwa chaguo namba moja kwa Arteta na mechi pekee ambayo Ramsdale alicheza ilikuwa kwenye michuano ya kombe la Carabao dhidi ya West Ham.

Ramsdale alikiri mwezi uliopita kwamba anaumia sana na kuteseka baada ya namba yake kupokwa lakini ameapa kupigania nafasi yake Arsenal.

Baba yake mzazi, Nick Ramsdale, amezungumzia kuhusu mustakabali wa mtoto wake huyo kwenye kikosi cha Arsenal akisema: "Aaron amepoteza tabasamu lake, ni ngumu sana tukimuona akiteseka kwa sababu tunapenda aendelee na tabasamu lake."

Nick kisha alifichua mazungumzo kati yake na Arteta na kudai kwamba kocha huyo alimweleza wazi kwamba Ramsdale ndio chaguo lake, licha ya wakala wa Raya hivi majuzi kusema kwamba kipa huyo aliwindwa kwa muda mrefu na Arsenal.

"Haiwezekani kwa jinsi mambo yanavyokwenda. Hatujui sababu ni nini. Ramsdale anafanya kazi kubwa sana Arsenal ishinde taji la ligi."

Pia akaongezea kwamba Ramsdale ambaye alikiri anapitia kipindi kigumu bado Arteta hajamwambia majukumu yake kwa sasa baada ya kupokwa namba.

"Ramsdale atakuwa kipa wa akiba tu, na Raya atakuwa chaguo namba moja labda kitu kitokee, majeraha au kutolewa."

Ramsdale aliongeza mkataba mpya wa muda mrefu wiki chache kabla ya Raya kusajiliwa kwa mkopo kipindi cha usajili wa kiangazi, huku Ramsdale akikubali uamuzi wa Arteta bila ya kufahamu mambo yatakuwa magumu.

# Southgate amchefua Ferdinand

**LONDON,** England

GWIJI wa soka wa England, Rio Ferdinand amemponda kocha Mkuu wa timu ya taifa ya nchi hiyo, Gareth Southgate baada ya kutomjumuisha winga wa Chelsea, Raheem Sterling kwenye kikosi chake.

Beki huyo wa zamani wa Manchester United alikasirishwa baada ya kocha kumpotezea Sterling kwa ajili ya mechi zijazo za kufuzu Euro 2024.

Rio alimkashifu Southgate akieleza kuwa nyota huyo wa Chelsea ametoa mchango mkubwa wa mabao msimu huu kuliko Jack Grealish na Marcus Rashford kwa pamoja.

Nyota huyo wa zamani wa Manchester City na Liverpool hajaichezea England tangu mechi ya robo fainali ya Kombe la Dunia dhidi ya Ufaransa Desemba mwaka jana.

Mchezaji huyo aliumia katika mechi za kwanza za kufuzu za Euro 2024 Machi mwaka huu, na baadae Southgate akampotezea mara nne mfululizo.

Akizungumza kwenye chaneli yake ya YouTube ya Five, beki huyo wa zamani wa England alisema: "Wamuachie huru Sterling. Mwachieni kijana wangu, Raheem Sterling. Sijui amefanya nini, sijui ni kitu gani kimetokea.

"Kukosekana kwake kwenye kikosi cha England inashangaza sana. Ndio kuna vipaji vingi sana, msinielewe vibaya. Lakini kama tunazungumzia kiwango, Sterling ana mabao mengi na asisti, na mchango mkubwa kuliko Rashford na Grealish kwa pamoja."

Vijana wa Southgate, ambao tayari wamekata tiketi ya kushiriki michuano ya Ulaya mwakani, jana walicheza dhidi ya Malta kabla ya kukabiliana na Macedonia ya Kaskazini keshokutwa.

Sterling amekuwa hatari kwenye kikosi cha Mauricio Pochettino kutokana na mchango wake, Chelsea ilipata matokeo chanya mechi za hivi karibuni ikiwamo sare ya mabao 4-4 dhidi ya Man City mwishoni mwa juma lililopita ambayo aliwasumbua sana mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England.



HABARI MICHEZO



# YANGA SC HAISHIKIKI KIPINDI CHA PILI LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Yanga kimeendelea kuonyesha ubora wao kipindi cha pili katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka kufikia raundi ya tisa kabla ligi haijasimama kupisha michezo ya timu za taifa.

Kwa mujibu wa dawati letu la takwimu na la Bodi ya Ligi, Yanga imefunga mabao 17 kati ya 26 iliyonayo mpaka sasa kipindi cha pili.

Hii ina maana Yanga wanaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania bara mpaka sasa, imefunga mabao tisa tu kipindi cha kwanza.

Takwimu zilizotolewa jana na Bodi ya Ligi zinasema kuwa Azam FC inashika nafasi ya pili kwa kupachika mabao mengi baada ya dakika 45 za kwanza, ikiwa imefanya hivyo mara 10.

**Azam ambayo ina mabao 19 ya kufunga, nayo kama Yanga imefunga mabao tisa kipindi cha kwanza.**

Prisons ipo kwenye nafasi ya tatu kwa kufunga mabao mengi kipindi cha pili, ikipachika mabao saba, huku mawili tu ikifunga kipindi cha kwanza katika mabao yao tisa ya kufunga kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

Nafasi ya nne inashikiliwa na Simba ambayo kwa mujibu wa takwimu zilizotoka juzi, inaongoza kwenye ligi mpaka sasa kwa kufunga mabao mengi kipindi cha kwanza, ikiwa imepachika mabao 12 kipindi hicho kati ya 18 iliyonayo mpaka sasa, hivyo imefunga mabao sita tu kipindi cha pili.

Timu za Dodoma Jiji, Singida Fountain Gate na Namungo ziko kwenye nafasi ya tano kwa timu zilizofunga mabao yake mengi kipindi cha pili, kila timu ikifanya hivyo mara tano sawa na timu za Namungo na Dodoma Jiji FC.



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk Damas Ndumbaro (kulia) akikabidhiwa jezi ya timu ya mpira wa Kikapu ya Pazi na Rais wa timu hiyo Musa Mzenji jana kabla ya safari ya timu hiyo kuelekea Afrika Kusini. **PICHA: SAADA AKIDA.**

# Wadau waendelea kuipongeza Karume Boys

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WADAU na Mashabiki wa Soka Visiwani hapa wameendelea kutoa pongezi kwa timu ya Taifa ya Vijana chini ya umri wa miaka 15, Karume Boys kwa kutwaa ubingwa wa kombe la michuano ya Afrika Mashariki na Kati inayosimamiwa na Baraza la soka la ukanda huo (CECAFA).

Wadau na Mashabiki waliungana na Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita katika viwanja vya Mnara wa Kisonge kufuatilia mchezo wa fainali kati ya timu hiyo na wenyeji Uganda uliochezwa juzi mjini Jinja.

Akizungumza na Nipashe Mwenyekiti wa Kamati ya Soka la Vijana Wilaya ya Mjini Unguja, Ali Said alisema kutwaa taji hilo hasa kwa timu za vijana inajenga ari kwa wachezaji wenye umri mdogo kupenda soka na kuchukulia kama sehemu ya kazi yao. Alisema tangu hapo awali soka la Zanzibar limetawaliwa na wachezaji wengi vijana ambao wanazaliwa na kukuwa katika mazingira ya kucheza mpira viwanjani na hata katika fukwe za bahari hasa forodhani .

Alisema licha ya kuwepo madaraja matatu ya Ligi za vijana hapa Zanzibar ambayo ni yale ya vijana chini yamiaka 17, miaka 15 na wale wa chini ya miaka 20 yanayosimamiwa na chama cha Soka Wilaya ya Mjini lakini bado jitihada zinahitajika kwa Serikali kuboresha zaidi Ligi hizo za vijana.

"Kwa muda mrefu Zanzibar tumekuwa na utaratibu wa Ligi za Vijana ambazo huchezwa kama ligi nyingine kwa kuzingatia umri wao na hii inatupa faida hasa pale inapohitajila timu ya Taifa ya vijana, makocha hawapati tabu na hawana haja ya kuzunguka na badala yake hujikita kafuatilia ligi hizi na kupata wachezaji wazuri, lakini lazima tuboreshe ligi hizi ili ziwe na nguvu pamoja na mvuto zaidi ili baadae tuweze kutengeneza vijana watakao tumikia timu kubwa ya Taifa ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla", alisema Saidi

Aidha, alisema ushindi huo wa Karume Boys ni moja ya mafanikio katika soka la Vijana visiwani humo na wengi wa vijana hao wana ndoto ya kuchezea timu kubwa ya taifa ya Zanzibar na Tanzania.

## Rungu la TFF lawaangukia Kibu, Diarra, Mwandebwa

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mkabaji wa Yanga, Khalid Aucho amefungiwa kucheza michezo mitatu na Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF) kwa kosa la kumpiga kiwiko mchezaji Ibrahim Ajibu wa Coastal Union, huku kipa wa timu hiyo, Djigui Diarra na winga wa Simba Kibu Denis wakipigwa faini kwa kosa la kwenda kushangilia mabao yao upande wa wapinzani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana jioni na Bodi ya Ligi, adhabu hizo pamoja na zingine zimetolewa na Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB), iliyokaa Novemba 14 kupitia mwenendo na matukio mbalimbali ya michezo iliyopita ya ligi.

Pamoja na mambo mengine, Kamati hiyo pia imemfungia miezi sita mwamuzi Emmanuel Mwandembwa aliyechezesha mechi kati ya Coastal Union dhidi ya Yanga iliyochezwa Novemba 8 kwa kile kilichosemwa kuwa ni kushindwa kutafsiri sheria 17 za mpira wa miguu jambo lililosababisha ashindwe kumudu mchezo huo uliochezwa Uwanja wa Mkwakwani Tanga, Yanga ikishinda bao 1-0.

Aucho, raia wa Uganda amefungiwa mechi tatu na kutozwa faini ya Sh. 500,000 kwa kosa la kumpiga kiwiko Ajibu kwenye mechi hiyo hiyo ya Coastal Union dhidi ya Yanga.

Kipa Diarra, raia wa Mali, ametozwa faini ya Sh. 500,000 kwa kusa la kwenda kushangilia mbele ya benchi la ufundi la Simba baada ya timu yake kufunga moja ya mabao yake dhidi ya Simba, mechi hiyo ilichezwa Novemba 5 Uwanja wa Benjamin Mkapa Yanga ikishinda mabao 5-1.

Aidha, winga wa Simba, Kibu, naye ametozwa faini kama hiyo ya Sh.500,000 kwa kosa kama hilo, kwani baada ya kufunga bao pekee kwa timu yake katika mechi hiyo, alikwenda kushangilia mbele ya jukwaa la mashabiki wa Yanga na kuonyesha ishara ya kuwafunga mdomo.

Kwa mujibu wa kamati hiyo, beki wa kati wa Simba, Mkongomani, Henock Inonga naye amepigwa faini ya Sh 500,000, ambapo yeye baada ya bao la Kibu, aliienda kushangilia mbele ya maofisa wa benchi la ufundi la Yanga.

Michezo
Jumamosi Novemba 18, 2023
Nipashe



UK. 21
Sancho ashikilia msimamo wake united

# AMROUCHE: KAZI IMEBAKI KWA WACHEZAJI

## Awataka wafanye kinachohitajika kuwapa furaha watanzania leo wanapoikabili....



**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa timu ya taifa 'Taifa Stars', Adel Amrouche amesema kwa maandalizi waliyoyafanya wana uhakika wa kupata matokeo mazuri kwenye mchezo wa leo dhidi ya Niger na kazi kwa sasa imebaki kwa wachezaji wenyewe.

**Taifa Stars leo itashuka kwenye Uwanja wa Marrakech nchini Morocco kucheza mechi ya kwanza kusaka tiketi ya kucheza Fainali za Kombe la Dunia mwaka 2026 katika nchi za Canada, Marekani na Mexico, itakapokwaana na Niger.**

Mechi hiyo ya Kundi E, inatarajiwa kuanza kuchezwa saa 1:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki.

Amrouche alisema jana kuwa ameandaa kila kitu, na amewaandaa wachezaji wake kufanya kinachohitajika na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, wanaweza kufanya kitu ambacho Watanzania watafurahi.

"Nawapenda sana watu wa Tanzania, na nataka kufanya kitu ili wafurahi na tumejiandaa kufanya hivyo, nataka wawe na furaha muda wote, tutakwenda uwanjani kufanya kila kinachowezekana kupata ushindi, najua kuna mapungufu kidogo lakini ni ya ndani na siyo ya mashabiki, najua tutacheza mechi mbili mfululizo Jumamosi na Jumanne kitu ambacho si kizuri sana kwenye mechi za kimataifa, baada ya mechi hii tutacheza dhidi ya Morocco, kwa mimi hakuna shida lakini kwa wachezaji ni tatizo kidogo ila tutakabiliana nalo," alisema Amrouche.

Aidha, alisema kwenye mechi ya leo wachezaji wake wamemuhakikishia kucheza kwa ajili ya taifa na wananchi wake, hasa wakizingatia Serikali imewapa sapoti kwa kutoa ndege maalum ya kuwapeleka Morocco na kuwarudisha.

"Tunamshukuru sana Rais wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutupa ndege, vinginevyo tungekuwa na safari ndefu sana, kwa usafiri wa Afrika kutoka Mashariki kwenda Magharibi ni mbali sana," alisema kocha huyo.

Ndege hiyo itawarudisha mara baada ya mechi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Jumanne kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Morocco.

Stars ipo Kundi E, pamoja na timu za Jamhuri ya Congo, Morocco, Niger, Zambia na Eritrea, ambapo timu moja ya juu itafuzu kucheza fainali hizo.

Ukanda wa Afrika kuelekea kwenye fainali hizo kuna makundi tisa yatakayotoa timu tisa kwenda kushiriki finali hizo za mwaka 2026.

# Simba, Yanga zafanyia kazi mapungufu haya

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

IKIWA imebaki wiki moja kabla ya michezo ya kwanza ya hatua ya Makundi ya Ligi ya mabingwa Afrika, Makocha wa Simba na Yanga kila mmoja ameanza kufanyia kazi mapungufu makubwa ya vikosi vyao kabla ya kuwakabili wapinzani wao.

Simba inayojiandaa kukabiliana na Asec Mimosas ya Ivory Coast Novemba 25, Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Daniel Cadena ameweka wazi kuwa moja ya maeneo ambayo ameyatolea macho kuhakikisha yanakaa sawa ni eneo ya ulinzi ambapo amesema safu hiyo imekuwa ikiruhusu magoli mengi.

Cadena, alisema licha ya safu yake ya ushambuliaji kujitahidi kufunga mabao, bado kuna mapungufu makubwa kwenye ulinzi.

Alisema haridhishwi na jinsi mabeki wake wanavyoruhusu mabao kwenye kila mechi kwani inasababisha hata timu ikifunga bao moja, bado kunakuwa na wasiwasi kwa benchi la ufundi, wachezaji na mashabiki pia.

"Kwa sasa kazi yangu kubwa kuelekea kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrikani ni kuisuka safu yangu ya ulinzi. Pamoja na kwamba bado sijakuwa nao wote kwani wengine wapo kwenye vikosi vya timu zao za taifa, lakini nataka kupunguza baadhi ya makosa na mapungufu na kuruhusu mabao, kwa timu kubwa kama yetu si vyema kuwa na tabia hiyo kwa sababu mara kwa mara tunacheza na timu kubwa ambazo hutumia makosa madogo kukuadhibu," alisema Cadena ambaye anakaimu nafasi hiyo baada ya Robertinho kutimuliwa kutokana na kipigo cha mabao 5-1 kwenye Ligi Kuu kutoka kwa Yanga wiki iliyopita.

Simba imeruhusu magoli kwenye mechi sita kati ya nane ilizocheza za Ligi Kuu.

Mechi ambazo haijaruhusu goli ni mbili ambazo ni ile iliyoshinda mabao 2-0 dhidi ya Dodoma Jiji na nyingine iliifunga Coastal Union mabao 3-0.

Aidha, kwenye mechi zote za Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la African Football League (AFL) Simba imeruhusu mabao.

Timu hiyo imeweka kambi Mbweni nje kidogo ya jijini la Dar es Salaam na inafanya mazoezi yake kwenye Uwanja wa Mo Arena, Bunju.

Kwa upande wa Yanga, Kocha Miguel Gamondi ameanza kufanyia kazi makosa ya wachezaji wake kupoteza nafasi nyingi za kufunga wanazozitengeneza.

Katika mazoezi ya timu katika kipindi hiki ligi ikiwa imesimama, Gamondi amekuwa akiweka mkazo kwa wachezaji wake jinsi gani ya kutumia nafasi hasa wanapofika kwenye eneo la mpinzani wao.

Wakiwa kambini Avic Town, Kigamboni, wachezaji wa Yanga wamekuwa wakifanya mazoezi ya kucheza soka la kasi kama kawaida yao, lakini Gamondi amekuwa akiwasisitiza kuutanua uwanja wanapokaribia eneo la hatari ili kuwavuta wapinzani na mipira kuingizwa ndani haraka na watakaokuwa wakiipata wazitumie nafasi zinazopatikana kuweka mpira nyavuni.

"Nahitaji wachezaji wote wafunge mabao kila mchezaji anapopata nafasi, mabao yetu mengi yamefungwa na viungo washambuliaji kuliko washambuliaji, hii ni nzuri kwa afya kwa timu, lakini pia nataka mabao yatoke sehemu zote, kwa washambuliaji na hata mabeki, kila anayepata nafasi afunge," alisema kocha Gamondi.

Yanga imefunga mabao 26 mpaka sasa ambayo kati ya hayo, mabao 20 yamefungwa na viungo washambuliaji na manne tu yamefungwa na washambuliaji huku mabao mawili yakifungwa na mabeki.

Yanga inajiandaa na mchezo wake wa kwanza hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CR Belouizdad ya Algeria utakaochezwa nchini humo Novemba 24.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >